SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




**Mwanafunzi** ahukumiwa miezi sita kifungo cha nje, kulipa faini kwa wizi

UKURASA 3



**Mbappe: PSG bado haijawa bora kwa sasa**

UKURASA 23


# Nipashe

Jumatatu Novemba 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580758

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Utekaji watu Lindi ulivyozua taharuki



• **Polisi**, viongozi wa vijiji, ndugu wa waliotekwa wathibitisha vitendo hivyo vinavyofanyika... *Endelea ukurasa 2*



Wananchi wa Kitongoji cha Ipiho Kijiji cha Namatunu, Kata ya Marika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wakiwa katika foleni ya kusubiri maji jana, yaliyozinduliwa na RUWASA wilayani humo, baada ya kijiji hicho kukosa maji ya bomba tangu nchi ilivyopata uhuru mwaka 1961. **PICHA: HAMISI NASRI**

## Wabunge: Serikali ipunguze ndege za kukodi

UKURASA 3




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi cheti cha udhamini wa mbio za Zanzibar Blue Economy, Kaimu Ofisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, ikiwa ni shamrashamra za sherehe ya kutimiza mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya nane. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Bunge labainisha mambo 10 ya kukuza sekta kilimo

UKURASA 2

**MICHEZO** NBC MARATHON ZAKUSANYA MIL. 200/- UK.22 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Pereira Ame Silima kuwa Balozi wa Tanzania wa Jamhuri ya Visiwa vya Comoro Ikulu ya Chwamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Utekaji watu Lindi ulivyozua taharuki

**Na Mwandishi Wetu ,** LINDI

WATU watano wilayani Lindi, wanadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana na kupelekwa kusikofahamika nyakati za usiku wakiwa majumbani mwao wamelala.

Tukio hilo lililothibitishwa na polisi, viongozi wa vijiji husika na ndugu waliotekwa, linadaiwa kutekelezwa usiku wa Oktoba 30, mwaka huu na kundi la watu wenye silaha za moto.

Wanaodaiwa kutekwa ni Ismaili Uwesu Yahaya, Shazir Mohamedi Chileu, M'baraka Ally Maliki, Hamisi Said Liendeko, wakazi wa Kijiji cha Rutamba ya sasa na Mussa Fukutu wa Kijiji cha Michee.

Wakazi wa maeneo yaliyotokea tukio hilo, Husna Mohamedi, Esha Mohamedi na Husna Issa, wamedai kwamba kundi hilo lilikuwa limevalia nguo za kiraia likiwa na bunduki na kwenda kwenye nyumba za watu hao kisha kuvunja milango na kuingia ndani, huku wakiwaamuru waume zao kufungwa pingu.

Imedaiwa kuwa watu hao walifanya upekuzi na kuondoka na vitambulisho zikiwamo kadi za benki na wanawake wakiamriwa kuendelea kulala bila ya kupiga kelele.

"Usiku tukiwa tumelala usingizi tukasikia milango ya nyumba ikivunjwa, tulipoamka tukaamriwa tukae kimya," alidai mmoja wa wanawake hao.

Pia walidai kitendo cha kutekwa kwa waume zao kinaendelea kuwapa wakati mgumu wa maisha, ikizingatiwa wana familia wakiwamo watoto wanaosoma. Abdulrahman Bakari Awadhi, Mwenyekiti wa Serikali ya Vijiji vya Rutamba ya sasa na Michee, amekiri wananchi wao kutekwa na kudai mpaka sasa hawajafahamu eneo walikopelekwa, licha ya kupita kuulizia vituo mbalimbali vya polisi.

"Vituo vya polisi kwetu Rutamba na Wilaya Lindi mjini tumefika kuulizia tumeambiwa hawana taarifa yoyote kuhusu hilo," alidai kiongozi huyo.

Alidai hilo ni tukio la pili kutokea mwaka huu, mwezi Januari 2021, watu wawili wanaume walitekwa na kupelekwa kusikojulikana na hawajarejea hadi leo.

Shaziri Mohamedi ni Katibu wa Chama cha Wananchi (CUF), alimwambia mwandishi wa taarifa hii kuwa waliokamatwa ni wanachama wa chama hicho na hafahamu sababu za kukamatwa kwao wala walikopelekwa.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Foka Dinya, alithibitisha ofisi yake kupokea taarifa hiyo, na kwamba wanaendelea kufuatilia ili kufahamu wanaohusika na matukio ya utekaji watu ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO… OF 2021
In the Matter of the Estate of the late PETER FRANK MGAZA of NTYUKA within Dodoma Region
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CAROLINA PETER MGAZA.

GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **08th Day of NOVEMBER 2021.**
Dated at Dodoma this **23TH Day of SEPTEMBER 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE



**KUPOTEA KWA KADI ZA GARI**

**LUCY GODFREY NGALLAWA** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina ya **ISUZU TRUCK,** yenye jina la **JOYCE JAMES** namba za usajili **T 772 ADF,** Chassis No. **1672692,** Engine No.**6BDI724661,** Na **ISUZU TXD55YTN** yenye jina la **GOODLUCK FRANCIS IMBOMA** namba za usajili **T 681 ADC,** chassis no. **2202201,** Engine no. **390823.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOM /DOM/RB/529674/2021.**


# Bunge labainisha mambo kumi kukuza kilimo

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limetoa mapendekezo 10 kwa serikali yanayopaswa kufanywa ili kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo na kuondoa umaskini nchini.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni serikali kuhakikisha inaongeza bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo kutoka Sh. bilioni 294.1 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 450 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Akiwasilisha bungeni taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti mwishoni mwa wiki, kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23, mwenyekiti wa kamati hiyo, Sillo Baran, alisema serikali inapaswa kuzingatia mapendekezo hayo ili kuinusuru sekta ya kilimo na kuondoa umaskini.

Baran alitaja pendekezo la pili ni serikali kuhakikisha inafanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba mbolea na pembejeo zinapatikana za kutosha kwa muda sahihi na kwa bei nafuu.

Lingine ni serikali kuondoa kodi, ada na tozo ambazo zinasababisha kupanda kwa bei ya pembejeo, mbolea na viuatilifu.

Pendekezo la nne ni serikali kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili taifa liwe na kilimo endelevu na cha mwaka mzima.

Alitaja pendekezo la tano ni serikali kutenga na kulinda maeneo kwa ajili ya kilimo, ufugaji na vyanzo vya maji kwa ajili ya kilimo.

Pendekezo la sita ni serikali kuanzisha na kuendeleza mashamba makubwa ya mazao yanayonunuliwa kutoka nje kama vile ngano, mafuta, sukari ya viwandani na shairi.

Saba ni serikali kuhakikisha kunakuwapo na maofisa ugani kutosha na vitendea kazi kama vile pikipiki na magari.

Alitaja pendekezo la nane ni kuwapo na ruzuku kwenye mbolea za kupandia, kukuzia mazao kutokana na mfumuko wa bei ya mbolea, serikali ichukue hatua kwa dharura kutoa ruzuku kwa mbolea angalau kwa bei nafuu ya mkulima isiyozidi msimu uliopita.

Pendekezo la tisa ni serikali kuchangamkia fursa ya uwapo wa masoko makubwa ya mazao ya mbogamboga, matunda na maua (horticulture) na la kumi ni serikali kuboresha kilimo cha umwagiliaji na mabwawa ya maji pamoja na uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora zinazovumilia ukame.

Baran ambaye ni Mbunge wa Babati Vijijini alisema sekta ya kilimo inachangia Sh. trilioni 44.08 sawa na asilimia 26.9 ya Pato la Taifa la Sh. trilioni 163.88.

Alisema jambo la kusikitisha ni kwamba sekta hiyo inaukuaji wa asilimia tatu hadi nne.

"Uchambuzi umebaini kwamba sekta zinazokuwa kwa kasi kama vile ujenzi (asilimia 14.4) ni kutokana na uwekezaji wa serikali katika sekta husika," alisema Baran.

Kadhalika, serikali ikifanya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kwa kuhakikisha inaendeleza kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na viuatilifu kwa bei nafuu, upatikanaji wa mbegu bora za mazao na mifugo na kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo.

Hatua hizo alisema zitaondoa umaskini kwa kiasi kikubwa kwa sababu sekta ya kilimo inatoa ajira kwa asilimia 66.3 ya Watanzania.

**HABARI KITAIFA**

# Mwanafunzi ahukumiwa miezi sita kifungo cha nje kwa wizi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAHAKAMA ya Wilaya ya Makete, mkoani Njombe imemhukumu mwanafunzi wa shule ya msingi mwenye umri wa miaka 13 kifungo cha nje cha miezi sita na kulipa faini ya Sh. 85,000 ndani ya siku 30 kwa mlalamikaji Sara Sanga (50), mkazi wa kijiji cha Lupalilo wilayani humo kwa kosa la wizi wa vitu mbalimbali.

Hukumu hiyo dhidi ya mshtakiwa wa kwanza, Anna Sanga (36) na mshtakiwa wa pili ambaye ni mwanafunzi ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Makete, Ivan Msaki.

Mwendesha mashtaka wa serikali katika kesi hiyo alikuwa Asifiwe Asajile.

Imedaiwa kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Septemba 4, 2021 majira ya saa tano asubuhi kwa mlalamikaji Sara Sanga (50), ambaye aliibiwa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 85,000 ambavyo ni mali yake halali.

Hata hivyo, upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha ushahidi dhidi ya mshtakiwa wa kwanza ambaye ni Anna Sanga.

"Mshtakiwa huyu amepatikana na hatia na amehukumiwa kifungo cha nje miezi sita kwa kosa la wizi kinyume na kifungu cha 258 na 265 cha sheria ya kanuni ya adhabu marejeo ya mwaka 2019," alisema Msaki.

**Hukumu hiyo dhidi ya mshtakiwa wa kwanza, Anna Sanga (36) na mshtakiwa wa pili ambaye ni mwanafunzi ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Makete, Ivan Msaki.**

# Wabunge wataka serikali kupunguza ndege za kukodi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KATIKA kuliimarisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Bunge limeitaka serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za kukodi ndege, ili shirika hilo liweze kukua na kujiendesha kwa faida.

Limesema mkataba wa ukodishaji wa ndege ulioingiwa kati ya Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) na ATCL unaitaka ATCL kuanza kulipa gharama za kukodi ndege baada ya kukabidhiwa ndege, hata kama ndege hizo hazijaanza kufanya safari zake.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti, Sillo Baran, aliyasema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23.

Alisema hatua hiyo iende sambamba na uwezekano wa kusamehe ada ya pango la ndege walau kwa miaka miwili kipindi ambapo athari za ugonjwa wa corona zilikuwa kubwa kati ya mwaka 2019/20 na 2020/21.

Mbali na hilo, Baran alisema serikali inapaswa kukamilisha haraka ujenzi wa viwanja vya ndege vya mikoa, ili kuongeza mtandao na idadi ya miruko ya ndege ya shirika hilo ndani ya nchi.

Alisema pia, serikali inapaswa kulipa madeni yaliyokuwa ya shirika hilo kabla ya kufufuliwa, ili kusafisha vitabu vya shirika.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 serikali ilitumia Sh. billioni 557.8 katika kuimarisha usafiri wa anga na ATCL.

Baran alisema kamati ilipata fursa ya kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi na kubaini changamoto ambazo zinakwamisha shirika hilo kusimama imara na kupunguza hasara.

"Kwanza kutokana na athari za ugonjwa wa corona shirika liliathirika, lakini hakukuwa na mpango wowote wa serikali kulinusuru shirika hilo kama yalivyo mashirika mengine ya ndege duniani, badala yake Wakala wa Ndege za Serikali aliendelea kutoza gharama ya pango kwa ndege zote hata zile zilizopaki kwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 1.5 kwa mwezi," alisema Baran na kuongeza:

"Aidha, Wakala wa Ndege za Serikali inaitaka ATCL kuweka amana ya matengenezo ya ndege yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.2 kila mwezi wakati matengenezo ya ndege yanafanywa na ATCL wenyewe na si wakala wa ndege za serikali".

Alisema pia kamati ilibaini kwamba mkataba wa ukodishaji wa ndege kati ya TGFA na ATCL unaitaka ATCL kuanza kulipa gharama za kukodi ndege mara tu baada ya kukabidhiwa ndege hata kama ndege hizo hazijaanza kufanya safari zake.

Baran alisema kamati pia ilibaini kwamba kasi ya kukamilisha viwanja vya ndege vya mikoa ni ndogo kuliko kasi ya kununua ndege.

Alisema pia kamati ilibaini kwamba asilimia 86.4 ya madeni yote ya ATCL mdai ni serikali.

# TAKUKURU yataka kibano rushwa kwenye VICOBA

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewataka wanachama wa VICOBA kuwa mstari wa mbele kupambana na vitendo vya rushwa ndani ya vyama vyao na kutoa taarifa wanapobaini kuna dalili za matukio hayo miongoni mwao ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi, wakati wa sherehe ya kufunga mwaka ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa VICOBA inayojumuisha vikundi 30 vilivyoundwa na watumishi wa TAKUKURU.

Taasisi hiyo inabebwa na dhamira isemayo, 'Tokomeza Umaskini, Kataa Rushwa ili ukue Kiuchumi.'

Alisema taasisi hiyo ina jukumu la kupambana na rushwa na wanapoona kuna watu wanawaunga mkono hawanabudi kuungana nao, ili kueleweshana zaidi lengo ni kuondoka vitendo hivyo katika nyanja zote.

"Ninawaunga mkono wanawake na wanaume wa Zuia Rushwa VICOBA, tunaamini wakipeana taarifa, elimu kuhusiana na rushwa inaturahisishia kupata taarifa, ushirikiano wakati tunafanya uchunguzi katika kutoa ushahidi au nyaraka ili tupunguze rushwa katika jamii," alisema.

Msumi alitoa wito kwa taasisi nyingine zinazofanya kazi kama hiyo ziunge mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan ya kupinga vita rushwa nchini.

"Wakumbuke wanayo nafasi ya kupinga rushwa kwa kutoa taarifa dhidi ya vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano au vielelezo vyovyote au kutoa taarifa inaweza isiwe moja kwa moja kwa ni rushwa lakini anaiona kwake haiko sawa aje tuna wataalamu tutaichambua na kujua ipo kundi gani," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Zuia Rushwa VICOBA, Bahati Kyajoba, alisema kila mwaka wanakutana na wanashirikiana na TAKUKURU wanapowaona baadhi yao hawako vizuri katika maadili hutoa taarifa kwa hatua zaidi.

"Kabla mwanachama hajaingia katika taasisi hii ni lazima ajitambue anatakiwa afanye nini, tunawafundisha kwanza kabla ya kujiunga. Ndani ya VICOBA kuna mchanganyiko wa wanawake na wanaume na watu wakiona wanaume wanashangaa, huwa tunawaelimisha wajue Vicoba siyo ya wanawake pekee," alisema.

Alisema baadhi ya majukumu ya taasisi hiyo ni kuwawezesha na kuwaelimisha wanachama kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika uendeshaji na utoaji wa huduma za vikundi na kufichua vitendo hivyo kama vipo.

Naye Mwanachama Abdulkarim Abdallah, alisema VICOBA vimemsaidia kukua kibiashara na amekutana na fursa ya viwanja.


**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamiziwa mrathi Na 101, 2021**

**Katika shauri la mirathi ya SELINA ANGOLWISE LUVANDA.....Marehemu**
**Wa KWIVAHA.**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na ALFRED GAMALIEL LUVANDA ......Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**

**(Kanuni ya 5(2) yakanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuudhuria katika shauri hili endapo wakita kakufanya hivyo mnamo tarehe ...14.......mwezi ...11..... mwaka... 2021..... kablaya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ,mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpakata rehetajwa hapo juu.
Zingatia;Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
*Marehemu hakuacha wosia
*Futa isiyohusika
Imetolewa leo tarehe...5.... mwezi ...11.... Mwaka...2021.....

HAKIMU MKAZI

116558402

**KUPOTEA KWA RESULT SLIP**



**HALIFA RICHARD MAINA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha sita yenye **index namba S2549/0715** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya ALPHA HIGH mwaka 2021,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **DAR/GOG/RB/511996/2021**

116558102

**KUPOTEA KWA PASSPORT**



**JOSEPH MUTAGIRWA LONGINO** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria **(Passport) yenye namba TAE 249101** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka **2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/528548/2021.**

116556402

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 44 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MARCEL SYLVESTER OLOMI**

**BY 1. JOYCE OLOMI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 24 day of 11....2021
Dated at Morogoro this 4 day of 11.....2021

RESIDENT MAGISTRATE

116557802

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 45 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late BENNY MATHIAS MWELA**

**BY 1. NEEMA KULILA SANJO**
**2. EDGA AGREY MWELA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 8 day of 12....2021
Dated at Morogoro this 4 day of 11.....2021

RESIDENT MAGISTRATE

116557902

# Miradi Liganga, Mchuchuma yaibuliwa tena bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, ameishauri serikali kumaliza haraka majadiliano ya muda mrefu na wawekezaji katika miradi wa migodi ya makaa ya mawe na chuma ya Mchuchuma na Liganga, ili Taifa liweze kukua zaidi kiuchumi.

Amesema majadiliano ya utekelezaji wa miradi hiyo yamechukua miaka mingi, hali inayoikosesha nchi mabilioni ya Shilingi pamoja na kukua kiuchumi.

Serikali inaendelea na mazungumzo na mwekezaji wa miradi hiyo iliyoko Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, ili kupata mwafaka wenye maslahi mapana na kuzingatia sheria za nchi katika miradi hiyo.

Miradi hiyo unganishi inajumuisha mgodi wa chuma Liganga wenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 2.9 kwa mwaka, kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma Liganga tani milioni 1.1 kwa mwaka, mgodi wa makaa ya mawe huko Mchuchuma wenye uwezo wa kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka. Miradi hiyo pia inahusisha kituo cha kufua umeme huko Mchuchuma cha Megawati 600, msongo wa kusafirisha umeme wa kilovoti 220 kati ya Mchuchuma na Liganga na Barabara kutoka Mchuchuma hadi Liganga.

Akichangia bungeni kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, Mwanyika alisema: "Majadiliano ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi hiyo yanaendelea miaka mingi na hayaishi. Yawezekana kuna ugumu katika majadiliano, lakini tufike mahali tufikie muafaka kwani uwekezaji katika miradi hii ni muhimu katika ujenzi wa Taifa."

Aliongeza: "Wachumi wanasema kuna gharama au kuna hasara ya kutofanya jambo fulani kwa wakati fulani. Sasa haya mazungumzo yamechukua miaka."

Alisema hivi sasa bei ya chuma duniani imekuwa kubwa, kwamba China pekee ndiyo wanatawala katika soko la uzalishaji wa chuma duniani.

Alisema China wanazalisha asilimia 56.5 ya chuma yote inayotumika duniani. Afrika inazalisha tani 17 lakini Tanzania inazalisha asilimia sifuri wakati chuma kipo.

"Wachina wamefanikiwa kutoa msaada duniani yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 462, kati ya hizo asilimia 80 imeenda kwenye miradi ya miundombinu, Afrika peke yetu tumepata misaada ya Dola za Marekani bilioni 106. Mnaweza kuona faida ya uzalishaji wa chuma," alisema Mwanyika.

Aliongeza: "Kuna haja kwa mpango huu kuangalia kwa mapana madai ya Mchuchuma na Liganga katika uchumi wa Taifa. Kama Tanzania tungeweza kuzalisha asilimia 20 ya chuma nina hakika bajeti yetu yote ingetoka kwenye biashara ya uzalishaji wa chuma. Tuone na tuna haja kila sababu haya majadiliano yanafika mwisho."

Mwanyika alisema endapo mwekezaji anasuasua ni wakati muafaka kwa serikali kuachana naye na kutafuta mwekezaji mwingine.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Spika wa Bunge, Job Ndugai, ambaye alisema: "Hili suala la Mchuchuma na Liganga limesemwa kwa miaka mingi sana. Ngoja tuone bajeti inayokuja kama serikali itasema chochote tujue tunafanya nini."

Ndugai alisema: "Hatujui nini kinaendelea, tumeiachia serikali muda mrefu, lakini majadiliano hayamaliziki, huenda wamekutana wanasheria tu hakuna wachumi. Tunataka kuwahi uchumi, ili nchi yetu ibadilike hapa ilipo, haya mataluma ya reli tunayojenga yangetoka kwenye chuma."

# Mil. 281/- zawalipa stahiki watumishi Mambo ya Ndani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ramadhani Kailima, amesema hadi kufikia Oktoba 21, 2021 Sh. milioni 281.73 zimetumika kwa ajili ya kulipia stahiki za watumishi.

Kailima, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kilichokuwa na lengo la kupitia utekelezaji wa mpango na bajeti ya wizara kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba 2021.

Alisema wizara itaendelea kuboresha stahiki mbalimbali za watumishi kadri bajeti itakavyoruhusu.

Pia katika mwaka huu wa fedha 2021/22 wizara imetenga Sh. milioni 96.18 kwa ajili ya kuajiri watumishi wapya 15.

"Tumeendelea kulipa watumishi stahiki mbalimbali na hadi kufikia sasa jumla ya Sh. bilioni 1.36 zimetengwa katika bajeti ya wizara kwa ajili ya kulipa stahiki mbalimbali za watumishi ikiwamo likizo, gharama za uhamisho, posho ya kukaimu madaraka, gharama za matibabu pamoja na gharama za mazishi kama yatatokea," alisema.

Vilevile, alitoa maagizo kwa baraza hilo kuzingatia utunzaji wa siri za serikali ambao hivi sasa watumishi wengi wanashindwa. "Kutunza siri maana kwa tafsiri ni jambo ambalo hupaswi kumwambia mtu ambaye hapaswi kujua kwa wakati huo, wala hupaswi kumwonyesha mtu.

"Taarifa sio lazima iandikwe secret ndio iwe ya siri, lakini taarifa ambayo hupaswi kumwambia Kailima wakati huo kwake ni siri hupaswi kumwambia, watumishi wengi tunataka kukwama katika hilo naomba niwasihi mtunze siri kwa kadiri mtakavyoona inafaa," alisisitiza.

Pia aliwataka kutumia mfumo rasmi kuwasilisha malalamiko kwa kuwa kipo kitengo na endapo wakishindwa waende ngazi ya wizara na ikishindikana waende nje ya hapo.

Aliwataka kutimiza majukumu na wajibu wao kwa wakati kutokana na wizara kuwa na vipaumbele na bajeti yake.

Vilevile, aliwaagiza watumie vikao vya idara na vitengo kuwasilisha taarifa za utekelezaji ili watu wajue hasa takwimu ili wizara nyingine ziige.

Kadhalika, alisema wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua changamoto zinazowakabili ili kuweka mazingira bora ya kiutendaji.

Hata hivyo, aliwataka kutumia kikao hicho kujadili taarifa pamoja na mada nyingine kwa uwazi na uhuru ili kuja na maazimio na mapendekezo yatakayosaidia wizara kutimiza majukumu yake kwa kuzingatia mpango na bajeti iliyowekwa.




Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akimkabidhi tuzo Meneja Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Alex Bitekeye, baada ya kampuni hiyo kushinda tuzo ya sekta binafsi yenye mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii kwenye wiki ya Azaki hivi karibuni jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkurugenzi wa zamani kortini tuhuma rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Magreth Nakainga (60), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita, kwa makosa mawili ya kula njama ya kutenda kosa na kutumia madaraka vibaya.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, kwa madai ya kutoa zabuni ya utengenezaji wa malisho ya mifugo eneo la Buhalahala kwa kampuni ya Runazi General Supplies Limited bila kibali cha bodi ya zabuni na kamati ya mipango na fedha kinyume cha sheria.

Awali, ilidaiwa mahakamani humo na wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Geita, Kelvin Murusuri akishirikiana na wakili Antidius Rutayuga,

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rutayuga, alidai kuwa kati ya Januari 7 hadi 26 mwaka 2015 katika Halmashauri ya Mji wa Geita mshtakiwa akiwa mkurugenzi kwa makusudi alikula njama na watumishi wenzake wawili kutenda kosa la kutumia madaraka vibaya. Rutayuga alidai kosa la pili mshtakiwa huyo alitumia madaraka yake vibaya kwa kutoa zabuni ya utengenezaji wa eneo la malisho ya mifugo Buhalahala kwa Kampuni ya Runazi General Supplies Limited, bila kibali cha Bodi ya Zabuni na Kamati ya Mipango na Fedha, kitendo ambacho ni kinyume.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alikana mashtaka na kupewa dhamana baada ya kukamilisha masharti ya kuwa na wadhamini wawili ambao waliwasilisha barua kutoka kwa mwajiri wao na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 3 kwa kila mdhamini.

Wakili huyo alidai kuwa upelelezi umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kusoma maelezo ya awali, ombi lililokubaliwa na Mahakama kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 2, mwaka huu.

# Wafanyakazi taasisi za fedha wasio na maadili kikaangoni

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imetangaza kiama na kuwachukulia hatua kali za kisheria baadhi ya wafanyakazi wa benki na taasisi za fedha wanaoshiriki katika vitendo vya ubadhirifu.

Baadhi ya vitendo hivyo ni rushwa wakati wa utoaji wa mikopo na kusababisha kuongezeka kwa mikopo chechefu na kutoza riba kubwa.

Miongoni mwa hatua ambazo benki hiyo imepanga kuchukua kwa wafanyakazi katika taasisi hiyo ya fedha ambao watabainika na kuthibitika kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu na rushwa katika utoaji wa mikopo au kushirikiana na wakopaji kufanya uhalifu huo ni pamoja na kuwafungia kuajiriwa na benki au taasisi yoyote ya fedha inayoendesha shughuli zake nchini.

Hatua nyingine ni kuwazuia kuajiriwa katika benki au taasisi yoyote ya fedha inayosimamiwa na BoT.

Kwa mujibu wa Gavana wa BoT, Prof. Luoga, wamebaini hilo, baada ya kufanya utafiti.

“Iwapo itathibitika kuwa kuna mfanyakazi wa benki anahusika katika kutoa mikopo bila kuzingatia taratibu, kukosa uadilifu na kushirikiana wakopaji katika kutoa mikopo kiuhalifu na vitendo vya rushwa, benki au taasisi husika ya fedha itatakiwa kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mfanyakazi huyo na Benki Kuu itamfungia kuajiriwa na benki au taasisi yoyote ya fedha inayoendesha shughuli zake nchini,”alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Luoga, kuongezeka kwa mikopo hiyo chechefu katika sekta ya benki ni moja ya sababu kubwa ya benki na taasisi za fedha kutoza viwango vikubwa vya riba za mikopo na kuhatarisha uimara wa sekta hiyo na kuathiri uchumi wa nchi.

Alisema baada ya kubaini hilo, BoT katika kuchukua hatua za kudhibiti vitendo vinavyochangia kuongezeka kwa mikopo hiyo chechefu pamoja riba kubwa, imepanga kuendelea kufanya ukaguzi wa benki na taasisi hizo ili kubaini sababu za kuongezeka kwa mikopo hiyo, na kwamba wafanyakazi ambao watahusika moja kwa moja na kadhia hiyo na ikathibitika, benki au taasisi ya fedha husika, itatakiwa kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi yao.

Alizitaka benki na taasisi za fedha ambazo wafanyakazi wake wana mikopo chechefu katika benki au taasisi za fedha nyingine kuwasilisha taarifa zao katika taasisi za kuchakata taarifa za mikopo.

Alisema BoT imetoa miezi mitatu kuanzia jana kwa wakopaji wote ambao hawajarejesha mikopo yao kufanya mipango ya kurejesha kabla majina yao hayajaingizwa katika rejesta maalum na benki au taasisi kupewa orodha hiyo.

**Kwa mujibu wa Prof. Luoga, kuongezeka kwa mikopo hiyo chechefu katika sekta ya benki ni moja ya sababu kubwa ya benki na taasisi za fedha kutoza viwango vikubwa vya riba za mikopo na kuhatarisha uimara wa sekta hiyo na kuathiri uchumi wa nchi.**

# TEC sasa kuifanya Tanzania ya kijani

**Na Richard Makore,** MWANZA

BARAZA la Maskofu Katoliki Tanzania (TEC), limezindua mpango wa miaka 13 kwa ajili ya kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuifanya Tanzania kuwa ya kijani. Uzinduzi huo ulifanyika jana jijini hapa katika mkutano uliokutanisha maaskofu wote wa Kanisa Katoliki nchini.

Katibu wa TEC, Padri Charles Kitima, alisema, mpango huo utahusisha pia serikali na utashirikisha jamii kwa ngazi zote kuanzia familia, kitongoji na kijiji.

Padri Kitima alisema sayari ya dunia iliumbwa na Mungu na kupewa mwanadamu kuitunza na mkakati huo utalenga kutunza mazingira kwa kupanda miti.

“Mungu aliumba dunia hii na kutupatia ili tuishi sasa ni jukumu letu kuitunza kwa kupanda miti,” alisema.

Alisema Tanzania ina watu milioni 60 na kila mtu akipanda miti mitatu na kuitunza itasaidia kutunza mazingira.

Aliongeza kuwa kila Parokia itatenga eneo kwa ajili ya kupanda miti pamoja na waumini wake watahimizwa kufanya hivyo.

Padri Kitima alisema watapeleka wataalamu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaotaka kupanda miti na kuitunza katika maeneo yao.

Aidha, alisema mwakani Tanzania itakuwa mwenyeji wa mkutano wa Maaskofu Katoliki 120 kutoka nchi nane za Afrika.

Alisema mkutano huo utazungumzia masuala yanayohusu mazingira ili kutoa hamasa kwa jamii bila kujali dini za watu.

Alisema maaskofu hao watatoka nchi za Sudan Kusini, Ethiopia, Zambia, Malawi, Uganda, Kenya, Eritrea na Tanzania ambao watakuwa na mkutano wa siku 10 Julai, 2022.

Awali, Rais wa TEC,Askofu Mkuu Gervas Nayisonga, akizungumza katika viwanja vya kanisani eneo la Kawekamo jijini Mwanza, alisema dhamira ya mkutano huo wa mwakani ni kuikumbusha jamii umuhimu wa kutunza mazingira.

Aliwaomba waumini wote wa kanisa hilo nchini kushirikiana ili kufaninikisha lengo hilo muhimu kwa nchi.

Aliwaomba wananchi kuendelea kupata elimu kuhusu utunzaji wa mazingira ili kufanya Tanzania kuwa mahala salama kwa ajili ya kuishi leo na siku zijazo huku kukiwa na hali ya hewa nzuri.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UTENGENEZAJI, UPIMAJI, USAMBAZAJI NA UTOAJI WA MABOMBA MAKUBWA YA HDPE**
**KUMBUKUMBU 0010007214**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya HDPE Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya ukuta wa HDPE kulingana na viwango na vipimo vilivyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Ukuta wa muundo wa Bomba za HDPE zitalingana kwa kuzingatia viwango EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

- Kuta za kila sehemu ya HDPE (2.45m) zitalingana na vipimo vifuatavyo.
- ID / DN1500 na kipenyo ch nje cha ukubwa 1630 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- ID / DN1800 na kipenyo cha nje cha ukubwa 1960 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- KAMPUNI ina haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabomba ya HDPE yaliyowekwa katika kiwanda cha uzalishaji cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001: 2015. Mfumo wa usimamizi wa ubora wa mtengenezaji utahitatakika kuwa uliothibitishwa kwa ISO 9001: 2015 na chombo cha uthibitisho cha Kimataifa.
- Malighafi inayotumika kutengeneza ukuta wa muundo wa bomba za HDPE na viunganishi vyake lazima vilingane na EN13476-1 / ISO 21138-1. Mahitaji ya ubora wa Bomba za HDPE na upimaji wao ni utahitajika kulingana na viwango EN13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake husika. Mahitaji ya ubora wa viunganishi zilizotengenezwa kutoka kwa muundo wa bomba za HDPE zitahitajika kulingana na EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake ya hivi karibuni.
- Mabomba yote ya HDPE yaliyotengenezwa kwa ukuta yatakayotolewa dhidi ya Zabuni hii "yatatiwa alama" kulingana na viwango vya sahihi vinavyotumika.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejeleo yajayo.

- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika. KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:

  Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa yo miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuwasilisha nia kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **09 Novemba 2021.**Kichwa cha Habari cha Barua Pepe kiwe ni **0010007214.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216553602

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars wakati wakuandika historia Kombe la Dunia ni huu

**KWA** mara nyingine tena timu ya soka ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Alhamisi wiki hii kuvaana na DR Congo kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar.

Huo utakuwa mchezo wa mwisho kwa Stars kucheza uwanja wa nyumbani katika hatua hii ya makundi ya michuano hiyo, kabla ya Jumapili wiki hii kwenda kufungia hesabu zake ugenini nchini Madagascar.

Katika michezo miwili iliyocheza nyumbani, Stars imeshinda mmoja dhidi ya Madagascar na kupoteza mmoja dhidi ya Benin, lakini ugenini imeshinda mmoja dhidi ya Benin na sare moja dhidi ya DR Congo.

Matokeo hayo yameifanya Taifa Stars kukaa kileleni mwa msimamo wa Kundi J ikiwa na pointi saba sawa na Benin inayozidiwa kwa wingi wa mabao ya kufunga huku DR Congo ikifuata kwa alama zake tano na Madagascar ikiburuza mkia kwa pointi tatu.

Hivyo, inachotakiwa kufanya Stars kwa sasa ni kuhakikisha inapata matokeo chanya Alhamisi dhidi ya DR Congo na si ushindi tu, bali na idadi kubwa ya mabao pia ili kuendelea kuikimbia Benin ambayo nayo Alhamisi wiki hii itakuwa nyumbani kuikaribisha Madagascar kabla ya kwenda ugenini kuvaana na Wakongomani.

Ikumbukwe kila kinara wa kundi kati ya makundi 10 kwenye michuano hiyo kwa Ukanda wa Afrika ndiye atakayevuka raundi ya kwanza na baada ya hapo itachezeshwa droo kwa timu hizo kucheza mechi moja ya mchujo nyumbani na ugenini ili kupatikana timu tano zitakazoliwakilisha bara la Afrika Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Kwa mantiki hiyo, hakuna kingine zaidi neno ushindi kwa Stars ili kuweza kupenya hatua hii ya awali, ambapo kama ikifanikiwa itaandika historia kwani hiyo itakuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kufika hatua ya mwisho ya mchujo ya kuwania kufuzu fainali hizo.

Tunaamini Taifa Stars inaweza kabisa kama wachezaji kila mmoja atadhamiria kujitoa kwa jamsho, lakini akiona fahari ya kuwa sehemu ya historia hiyo mpya kwa Tanzania kwenye michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya dunia.

Kikubwa kwa sasa ni wachezaji kumulika mchezo huo dhidi ya DR Congo na kisha kuhamishia hesabu zao dhidi ya Madagascar kwa kwenda kupigana kufa au kupona ili kutinga hatua ya mwisho ya mtoano.

Tunachokitaka sisi ni kuona kwanza Stars inaibuka kinara wa Kundi J na kama itafanikiwa kwa hilo, hatuna shaka kabisa kwa hatua inayofuata kwani tunaamini utakuwa mwaka wa Tanzania kuishangaza dunia.

Ndiyo tunasema hivyo hasa tukitambua mechi hizo mbili hatua ya mwisho za mtoano nyumbani na ugenini, huwa hazina mwenyewe na inategemea siku nzuri za wachezaji kulingana na walivyoamka, hata kama Stars itaangukia dhidi ya miongoni mwa vigogo wa Afrika, bado lolote linaweza kutokea na kuishangaza dunia kwa kufuzu kwa mara ya kwanza fainali hizo.

Kwa sasa Watanzania hawana budi kutumia vema nafasi ya mashabiki 30,000 ambayo Shirikisho la Soka Afrika (CAF) limeruhusu kuingia uwanjani kushuhudia mchezo huo dhidi ya DR Congo ili kuwapa wachezaji wetu sapoti ya kutosha.

Katika hilo, mashabiki wa soka na Watanzania kwa ujumla hatuna budi kuchangamkia tiketi hizo ili kwenda uwanjani kwa wingi kuhakikisha tunaitumia vema nafasi ya kuwa mchezaji wa 12 kwa kushangilia Stars mwanzo mwisho kuchagiza kupata ushindi. Kila la Kheri Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji wazawa wanakwama wapi kwa ufungaji?

Na Adam Fungamwango

**KATI** ya wachezaji tisa wanaoongoza kwa kuwa na mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, sita ni Watanzania, hiyo inamaana watatu ni wakigeni na wote wana mabao mawili kila mmoja.

Wachezaji hao ni Fiston Mayele na Jesus Maloko wa Yanga, na Meddie Kagere wa Simba. Mayele na Jesus wanaochezea timu moja ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, huku Kagere akiwa ni Mnyarwanda.

Anayeongoza kwa kupachika mabao mpaka sasa ni Mbongo, naye ni Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania ambaye ana mabao manne mpaka sasa, Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye raundi ya tano. Anayefuatia pia ni mchezaji wa Kitanzania, Feisal Salum 'Fei Toto' wa Yanga, mwenye mabao matatu mpaka sasa.

Wachezaji wenye mabao mawili kila mmoja wa Kitanzania, ukiondoa watatu wa kigeni ni Reliants Lusajo na Shiza Kichuya wa Namungo FC, Ramadhani Chombo 'Redondo', na Chrispin Ngushi wa Mbeya Kwanza.

Hapa nilitaka niweke wazi kuwa mpaka kufikia raundi ya tano ya Ligi Kuu, wachezaji wa Kitanzania wanatamba kwenye orodha ya msimamo wa Ligi Kuu. Wameanza vizuri kuliko wakigeni.

Tatizo la wachezaji wa Kitanzania linakuwa ni mwendelezo. Wala si ajabu orodha hii ya wachezaji ikakomea hapo, na hawa watatu wa kigeni, wakakwea juu na kufukuzana kuwania Kiatu cha Dhahabu.

Unaweza kukuta pia hata wale ambao hawajaanza vizuri msimu huu au majeruhi wakawakuta wachezaji wa wazawa wakiwa na mwendo wa kinyonga kama si wa kobe na kuwapita.

Kuna mastraika kama Chris Mugalu wa Simba na Prince Dube wa Azam, ambao ni majeruhi, wanaweza kupona, wakarejea uwanjani na kuwapa wakati mgumu wachezaji wazawa kwenye ufungaji bora.

Nina wasiwasi hiyo kwa sababu huko nyumba imetokea. Hawa hawa, Mugalu na Dube walikuwa majeruhi msimu uliopita. Wakacheza mechi chache sana, lakini ilikuwa nusura wachukue Kiatu cha Dhahabu.

Mugalu alikosa ufungaji bora kwenye mechi ya mwisho, akizidiwa bao moja tu na mzawa, John Bocco. Bocco alitumia uzalendo kwa kufunga bao kwa mkwaju wa penalti kwenye mechi dhidi ya Namungo, ikiwa ni ya mwisho wa msimu uliopita, Simba ikishinda mabao 4-0.

Alimaliza akiwa na mabao 16, Mugalu akiwa na 15 kama Dube, na mwenye mabao 13 alikuwa ni Kagere. Hapo utaona kuwa ligi ilimalizika wageni wakiwa juu, watatu dhidi ya mmoja mzawa, Bocco.

Ni yeye pekee ambaye tangu msimu wa 2008/09, ndiye anayeonekana kumaliza akiwa kwenye mstari wa juu wa wafungaji bora.

Kuna sehemu wachezaji wa Kitanzania wanakwama. Sijui wanakwama wapi, haiwezekani wanaanza mbio za ufungaji bora vizuri kuliko hata wachezaji wa kigeni, lakini mwisho wa siku, hata kama Mtanzania akibahatika kuwa mfungaji bora, atafuatiwa au kukabwa koo na wachezaji wengi wa kigeni. Na hata akiwa mgeni, wanaomkaba koo watakuwa wageni, wenzake na Watanzania watakuwa wachache. Mwendelezo wa ufungaji kwa wachezaji wa Kitanzania umekuwa tatizo kubwa kwao.

Ukiangalia pia hata wanaobahatika kutwaa ufungaji bora, msimu ujao wanapoteza, na si kwenye ufungaji bora tu, hata tano bora wanakuwa hawapo kabisa.

Ni Bocco tu ndiye anayeweza kufanya hivyo.

Tulitegemea Salum Aiyee, aliyekuwa nyuma ya Kagere msimu wa 2018/19, atatisha msimu unaofuata, akapotea. Waziri Junior na Yusuph Mhilu wakimfuatia Kagere msimu wa 2019/20, lakini kila mtu anafahamu kilichowatokea. Junior alichukuliwa Yanga, akapotea, na sasa ameshaondoka, Mhilu yupo Simba na hajafunga bao lolote mpaka sasa.

Mohamed Rashid, Marcel Kaheza, Habib Kyombo, Elius Ambukile, walimsumbua sana Emmanuel Okwi alipochukua Kiatu msimu wa 2017/18. Wapo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, lakini makali yao si yale tena.

Abdurahman Musa wa Ruvu Shooting alichukua Kiatu cha Dhahabu 2016/17, kwa sasa anamaliza msimu akiwa hafiki hata kumi bora. Mifano ni mingi sana.

Cha kujiuliza tu, wachezaji wazawa mbona hawana mwendelezo kwenye ufungaji bora! Wanakwama wapi?

HABARI KITAIFA

# Kidato cha nne wapewa mbinu ufaulu

**Na Mary Geofrey**

WITO umetolewa kwa wanafunzi wanaotarajia kufanya mitihani ya kidato cha nne, Novemba 15, mwaka huu, kuzingatia malengo yao na kuepuka kujaza madudu.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mwasisi wa Shule ya Sekondari Huria ya Skilful, Diodorus Taboro, katika mahafali ya 15 ya kidato cha nne.

Alisema wanafunzi wengi hawaziishi ndoto zao hasa wakati wanapokuwa wanafanya mitihani ndio sababu ya kuamua kujaza wanavyojisikia.

"Msikimbilie kujaza mitihani kwa sababu tu mnataka kumaliza shule. Hakikishe mnajaza kikamilifu kile mlichojifunza," alisema Tabaro.

Aidha, aliwataka wazazi kushirikiana na walimu wa wanafunzi ili kusaidia kufuatilia mienendo yao, kuwaepusha na tabia za makundi rika ili wajikite kwenye masomo. "Shule yetu imekuwa ikimtegemea Mungu kwa mambo yote tunayoyafanya, hivyo nawahasa vijana hawa kuendelea kumtegemea Mungu katika mitihani yao na kuamini wanafanya vizuri zaidi," alisema Tabaro. Tabaro alisema shule yao imekuwa ikipokea wanafunzi ambao tayari wamekata tamaa na wengine hawamalizi shule.

"Unajua wanafunzi tunaowapokea ni wale waliokata tamaa, walioishia njia na waliofeli, tunawachukua na kuwapa mafunzo maalum ya kujitambua.

"Baada ya hapo sasa ndio wanaanza kuwapa masomo ya darasani, hii huwasaidia akili zao kuchangamka na kujiweka tayari kupokea wanachofundishwa," alisema.

Mmoja wa wahitimu wa shule hiyo, Lukuman Emmanuel, alisema amejipanga vizuri kufanya mtihani wake huo wa mwisho kwa sababu wameelekezwa namna ya kujiamini na kuwa watulivu wanapofanya mitihani.

"Natarajia nitafaulu vizuri mitahani yangu hasa kwa kuzingatia kuwa nilikuwa na muda mrefu wa kujiandaa na sitaki kurudia makosa niliyofanya nyuma nikafeli," alisema Lukuman.



Mwanafunzi bora kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka huu, Eluleki Haule akionyesha cheti alichokabidhiwa na shule yake ya St Anne Marie kumshukuru kwa kushika nafasi hiyo kwenye hafla ya kumpongeza iliyofanyika mwishoni mwa wiki Mbezi Kimara kwa Msuguri Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mshindi kitaifa darasa la 7 kusomeshwa bure

**Na Joseph Mwendapole**

MWANAFUNZI aliyeongoza kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba, Eluleki Haule, ameula baada ya shule aliyosoma ya St Anne Marie Academy kuahidi kumsomesha bure hadi kidato cha sita.

Ahadi hiyo ilitangazwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza, wakati wa hafla iliyoandaliwa na shule hiyo kumpongeza kutokana na ushindi wake.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera, Constansia Buhiya na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Kheri James.

Dk. Rweikiza alisema mbali na kumsomesha bure, shule hiyo itampa Sh. 3,000,000, kumpeleka kumtambulisha bungeni Dodoma yeye na wazazi wake na kubandika picha yake kwenye magari yote 51 ya shule hiyo.

Aliwataka wanafunzi wahitimu kuacha kubweteka huku akiwasisitiza kusoma na kujituma kwa bidii ili waweze kufanya vizuri katika kasomo yao na mitihani kwa ujumla.

"Niwashukuru walimu kwani walipambana sana hadi kufanikiwa kupata mafanikio haya, pia nimshukuru mkuu wa shule kwa uongozi bora pamoja na wanafunzi wote waliofanikiwa kufanya vizuri katika mitihani yao na niwasisitize mwendelee kusoma kwa bidii kwani taifa linawategemea," alisema Rwaikize.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, alimpongeza mwanafunzi huyo na kumtaka aendelee kufanya vizuri kwenye masomo yake ya sekondari.

Alisema kwa matokeo hayo ni ishara kwamba wazazi na walimu wanatimiza majukumu yao huku akitoa wito kwa wazazi walezi na jamii kuwalea watoto katika maadili mema na kutoa kipaumbele kwenye elimu ili baadaye wajisaidie na kulisaidia taifa kwa ujumla.

"Kwa niaba ya serikali tunampongeza kijana Haule kwa kuwa Tanzania One kwa mwaka huu. Leo Tanzania nzima wanaijadili St. Anne Marie kwasababu ya mtoto huyu, hii ni safari ya kwanza ambayo umeanza tunatarajia utafanya vizuri zaidi katika ngazi zinazoendelea," alisema James.

## GGML yadhamini matibabu wagonjwa midomo sungura

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Rafiki Surgical Mission ya Australia mwaka huu imeendeleza udhamini wake wa kusaidia kugharamia upasuaji na matibabu ya wagonjwa wagonjwa 25 wa midomo sungura.

Upasuaji na matibabu ya wagonjwa hao umefanyika katika Hospitali ya Sekou Toure jijini Mwanza mwezi huu.

Msaada huu umekuwa ukitolewa kwa zaidi ya muongo mmoja hivi sasa tangu mwaka 2002 ukitoa matibabu kwa wangojwa zaidi ya 1,717 wakiwamo watoto na watu wazima kutoka maeneo yanayozunguka mgodi.

Midomo sungura ni changamoto ya kidunia na bahati mbaya ni tatizo linalowakumba zaidi watoto wa kuzunguka eneo la Ziwa Victoria ambapo GGML inapatikana.

Chanzo cha midomo sungura hakijulikani, lakini inasemekana ni matokeo ya jeni na sababu za kimazingira. GGML inatoa udhamini huu ili kurejesha matumaini na tabasamu kwa watoto na watu wazima, ambao watagharamiwa matibabu, malazi na usafiri katika kipindi chote ambacho watapatiwa matibabu hayo.

Meneja uendeshaji wa GGML, Wayne Louw, alisema udhamini huo unaendana na tunu na ahadi za kampuni yake ambapo afya ni kipaumbele cha kwanza cha kusaidia jamii inayozunguka mgodi.

Lauw alisema katika kipindi cha miaka 17 ambayo GGML imegharimia matibabu hayo, wagonjwa wote waliofanyiwa upasuaji wamepata matumaini mapya na maisha yao yamekuwa tofauti kabisa.

Alisema GGML imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo mkoani Geita na kwa kushirikiana na serikali imefanikiwa kuwekeza kiasi cha Sh. bilioni 50 kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo ya afya, elimu na miundombinu.

Aidha, alisema Kampuni ya GGML pia imelipa zaidi ya Sh. trilioni 3.9 kama kodi ya serikalini tangu kuanza shughuli zake mwaka 2000. Mbali na kodi na fedha za wajibu wa kampuni kwa jamii, kampuni pia inao mpango wa kusaidia fursa za kukuza uchumi kwa wafanyabiashara wazawa, ambapo imetumia Sh. bilioni 67.6 katika manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa kampuni za kitanzania mwishoni mwa Septemba 2021.

# TWCC yazindua mradi kuwainua wanawake

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), kimezindua mradi wa kuwajengea uwezo wanawake ili kuwaongezea ujuzi na ushindani katika sekta ya nguo na ubunifu wa mavazi.

Akizindua mradi huo jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Sila, alisema lengo kubwa ni kuhakikisha wanawaongezea ushirikiano kwenye sekta hiyo kuzalisha bidhaa bora na kufikia masoko.

"Tunataka kuona tunazalisha wabunifu wakubwa ndani ya TWCC na tunatamani kuona wanapata masoko ya uhakika kwa kuzalisha na kuboresha bidhaa zao ili zishindane kitaifa na kimataifa," alisema.

"Mradi huu umeanza kwa kuchukua wanawake 35 kutoka mikoa mbalimbali nchini na kama watautumia vizuri, zipo fursa nyingi ambazo watanufaika nao ikiwamo kuuza bidhaa zao kwenye maonyesho makubwa ndani na nje ya nchi na mpaka sasa kuna fursa ya soko la uhakika nchini Marekani."

Alisema TWCC imeanza kufanya kazi kupitia kongani ili kuhakikisha wanawake walio katika sekta zinazofanana wanakuwa na mtandao wao popote walipo nchi nzima.

"Nitoe wito kwa wanawake wajasiriamali ambao wamepata nafasi ya kushiriki katika mradi huu, kutumia vizuri nafasi waliyopata ili kuboresha biashara zao zishindane kitaifa na kimataifa," alisema Sila.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, alisema mradi huo umefadhiliwa na Shirika la GIZ la Ujerumani na kwamba wanaamini utawasaidia wanawake hao kwa kiwango kikubwa kuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa za kiushindani na kufahamu namna ya kutafuta masoko.

"Wote tunafahamu umuhimu wa hii sekta ya ubunifu wa mavazi, inahusisha watu wote wenye elimu na wasio na elimu, takwimu zinatuambia baada ya sekta ya kilimo ambayo inaajiri watu wengi, inayofuata kwa wanawake ni hii ya mavazi," alisema.

"Eneo ambalo linabebea watu wengi hususani wanawake na tunaamini kwamba wakifanya vizuri zaidi katika eneo hili watachangia kwa kiwango kikubwa kwenye pato la taifa na watakuza kipato binafsi."

Naye Mwakilishi kutoka GIZ, Lydia Koch, alisema wameamua kufadhili mradi huo kupitia mradi wa 'Business Scouts for Development' ambao unatekelezwa katika nchi zaidi ya 40 na kwamba lengo ni kutoa mafunzo na kusaidia kukuza viwanda na kuwezesha watu binafsi mbinu za kusimamia biashara zao.



Mwakilishi wa Asasi ya Kiraia ya HakiElimu, Lucy Karage, akitoa maelekezo kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia kwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwenye warsha ya siku mbili ya uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya halmashauri iliyofanyika jana Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Makandarasi waonywa mzaha kazini

**Na Joseph Mwendapole, aliyekuwa,** IRINGA

MSAJILI wa Bodi ya Makandarasi nchini (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori, amewataka makandarasi kuacha tabia ya kutumia fedha za miradi kufanya matanuzi kabla ya miradi hiyo kukamilika.

Alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akifunga mafunzo kwa makandarasi wazalendo wa mikoa ya Iringa, Njombe, Dar es Salaam, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Tanga, Morogoro, Mwanza na Ruvuma iliyofanyika mkoani Iringa.

Alisema kazi ya ukandarasi ni biashara inayohitaji mipango na usimamizi wa fedha kwa kufuata maadili ya kazi ili kujenga uaminifu wa kupata kazi zingine kwa wateja wao badala ya kutumia fedha kabla ya mradi.

"Huwezi kupata faida kabla ya mradi kukamilika na Ili upate faida lazima ukae kwenye ratiba uliyojiwekea na kufanyakazi kwa malengo uliyojiwekea na kuna faida kubwa kukamilisha mradi mapema kwa sababu unaokoa gharama nyingi za kulipa wafanyakazi na mashine ulizokodi," alisema Nkori.

Aliwataka makandarasi kuheshimu mikataba wanayoingia na wateja wao ikiwamo kuepuka matumizi ya fedha za miradi nje ya shughuli kabla ya kumaliza miradi husika. "Unapopewa mradi uheshimu kwasababu wengi wetu tunapewa pesa za miradi tunatumia hizo hela kwa mambo yetu binafsi kabla ya mradi kuanza jambo ambalo linasababisha wakati mwingine kupata hasara na mradi kutomalizika kwa muda na ubora uliopangwa," alisema.

Mmoja wa makandarasi walioshiriki mkutano huo, Emmanuel Mshana, kutoka kampuni ya ukandarasi ya LABA ya jijini Dar es Salaam alisema, mafunzo hayo yamekuwa msaada mkubwa kwa makandarasi.

"Tumejifunza namna yakuandaa mpango kazi, kusimamia mikataba yetu na jinsi ya kutumia mfumo wa kuwasilisha zabuni kwa njia ya kielektroniki TANePS," alisema.

Naye Osward Kikoti ambaye ni mkandarasi aliishukuru CRB kwa kuwapatia mafunzo hayo na kusema kwa sasa wanajua nini cha kufanya wanapoingia mikataba na kukutana na changamoto mbalimbali.

"Kwa kweli, TANEPS imetusaidia kwa kiasi kikubwa sana kulinganisha na zamani ambapo sasa inatusadia matumizi ya muda na kuepuka mlolongo mrefu wa kufikisha zabuni yako kwa kuwa ukitumia mtandao kazi yako inafanyika mahali popote pale," alisema.

# Wanakijiji walivyojenga sekondari kwa nguvu zao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kijiji cha Mmangu Salawe wilayani Shinyanga, wamejenga shule mpya ya Sekondari kwa nguvu zao wenyewe, ili kuondoa adha ya watoto wao kusoma umbali mrefu katika Shule ya Sekondari Salawe.

Ofisa Elimu Kata ya Salawe, Joseph Kulwa, alibainisha hayo wakati Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa madarasa matatu katika shule hiyo mpya ya Sekondari Mmangu, kufuatilia utekelezaji wa fedha ambazo zilitolewa na serikali Sh. milioni 60.

Alisema wananchi hao baada ya kuona watoto wao wanasoma umbali mrefu, ndipo wakaamua kuanzisha shule hiyo kwa kujenga madarasa sita, matundu ya choo nane na ofisi ya walimu.

"Mkuu wa Mkoa kijiji hiki kinatoa wanafunzi wengi sana kwenda sekondari, mfano matokeo ya mwaka huu darasa la saba ambapo wanafunzi wataingia mwakani kidato cha kwanza ni 477, ambapo kijiji hiki kimetoa wanafunzi 280," alisema Kulwa.

"Kufuatia ujenzi wa shule hii mpya ya sekondari ambayo tunatarajia mwakani ianze kufanya kazi, licha ya kupunguza umbali wa wanafunzi kwenda shule, pia itapunguza na mlundikano madarasani, ambapo wanafunzi wataelewa masomo na kufanya vizuri," aliongeza.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alipongeza wananchi kwa kujenga shule kwa nguvu zao wenyewe, na kubainisha katika ujenzi wa madarasa hayo matatu ambazo fedha zake zimetolewa na Rais Samia, Suluhu Hassan kutafanya kuwa na madarasa tisa.

Aidha, alitoa hamasa kwa wananchi wa kijiji hicho, kuwajenge na hosteli kwa ajili ya kuwalinda wanafunzi wa kike kutokatisha masomo yao kwa sababu sababu ya kurubuniwa na kupewa ujauzito na kuzima ndoto zao.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Mkoa, aliagiza ujenzi wa madarasa hayo matatu kasi yake iongezeke ili yakamilike kwa wakati, kwa kuwa amesaliwa na mwezi mmoja tu.

Nao baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, walisema walihamasika kujenga shule hiyo mpya kutokana na watoto wao kupata shida ya kusoma umbali mrefu, huku watoto wa kike wakitongozwa njiani, na wengine kuambulia ujauzito na kuacha masomo.

## Kichocheo magonjwa yasiyoambukiza hiki

**Na Christina Mwakangale**

MFUMO wa maisha na lishe duni vimetajwa kuhatarisha maisha kutokana na kuwa kati ya sababu za magonjwa yasiyoambukiza, hususan kwa wakazi waishio mijini.

Hayo yamebainika baada ya wakazi 25 kati ya 123 sawa na asilimia 20 ya wakazi hao, waliofika kupima afya zao walibainika kuwa na shinikizo la juu, huku 28 wakiwa na uzito uliozidi na kuhatarisha afya zao ikiwamo kuugua ugonjwa wa kisukari.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dk. Milka Mathania, aliyasema hayo kwenye kongamano la Siku ya Mtoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Duniani, iliyokwenda sambamba na kufanya vipimo vya bure vya kiafya kwa wakazi wa mkoani hapa, ikiwamo kutoa elimu ya kujikinga na magonjwa hayo.

Alibainisha kwamba, waliobainika kuwa na maradhi kati yao hawakufahamu wanaugua maradhi yasiyoambukiza kutokana na kutokuwa na utamaduni miongoni mwa wanajamii, kupima afya zao mara kwa mara.

Kadhalika, Dk. Milka alibainisha kati ya wakazi hao 68, walibainika kuwa na lishe bora huku watatu wakibainika wanaugua kisukari.

## Taasisi yawanoa wanafunzi kimaadili

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Kijamii ya Community Hands Foundation (C-FH), imezindua mradi wa Elimika unaolenga kuimarisha na kutoa elimu ya afya na maadili kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili kujiepusha na utovu wa nidhamu.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi huo uliofanyika katika Shule ya Mshingi Mchikichini jijini Dar es Salaam, Mkurungezi wa (C-FH) Paul Makoe, alitoa wito kwa wadau wa maendeleo nchini kuunga mkono juhudi za kutafuta suluhu za matatizo ya kijamii.

Pia lengo jingine ni kuwafundisha watoto na vijana kuhusu afya, maadili na malezi, na kwamba utafiti ndogo waliyoifanya walikutana na malalamiko kutoka kwa walimu na walezi juu ya uwapo wa upotovu wa maadili kwa wanafunzi.

"Mradi huu utaendeshwa kwa muda wa miaka mitano na tunatarajia kufikia zaidi ya mikoa 20 nchini, hivyo tunaomba wadau wa elimu na taasisi mbalimbali kujitokeza kuunga mkono juhudi hizi ili kuhakikisha jamii inapata uelewa kamili," alisema Makoe.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Erenest Kibwinya, alisema elimu hiyo imekuja wakati muafaka kwa kuwa itasaidia idadi kubwa ya vijana kuepukana na vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa maadili.

"Niipongeze taasisi hii kwa kuliona tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu na kuamua kulishughulikia, hilo litasaidia kuleta mabadiliko chanya kwa watoto wetu," alisema Kibwinya.

# Vijana wazawa walivyokuja na ukombozi kwa wafanyabiashara

**Na Romana Mallya**

VIJANA wazawa Emmanuel Kimaro na Abbas Mussa, waliohitimu masomo yao mwaka 2015 katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), wamebuni mfumo wa kusaidia wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa wa kusimamia mwenendo wa biashara na kujua faida na hasara na tayari kampuni 231 zimeanza kuutumia.

Emmanuel ana Shahada ya Biashara ya Teknolojia ya Habari na Abbas ni Mhandisi wa kompyuta ambao kwa pamoja wameanzisha mfumo huo kupitia kampuni ya Fintech Start Up unayojulikana kama Bizzyn.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana vijana hao ambao tayari wametoa ajira kwa vijana wenzao 15 huku wakihitaji wengine kwa ajili ya mauzo kupitia Bizzyn, walisema baada ya kubuni mfumo huo mwaka jana unaoangalia mwenendo mzima wa biashara, walianza kwa majaribio kwa kampuni 10 na kuonyesha matokeo chanya na ndipo mwaka huu ulipozinduliwa rasmi.

Kimaro alisema walianza kwa mtaji wa Sh. milioni 10 fedha ambazo zilitokana na kuwa miongoni mwa washindi wa mashindano ya ujasiriamali yanayoendeshwa na Benki ya Stanbic na sasa wanatafuta wawekezaji watakaowezesha kupatikana Sh. milioni 80 ili waweze kukua zaidi na kusambaza mfumo ndani na nje ya nchi.

"Kwa nini mfumo huu, wakati tupo katika mafunzo kwa vitendo na wenzangu, tuliona namna kampuni zinavyopata shida katika kutunza kumbukumbu zake za biashara na wengi tuliona wanatunza kwenye makaratasi na ili kupata kitu wanachokihitaji tuliona wanatumia muda mrefu," alisema.

Alisema baada ya kuona tatizo hilo ambalo limechangia pia baadhi ya wafanyabiashara kufunga biashara zao kutokana na kuzifanya bila ya kujua mwenendo wake, ndipo wakaamua kubuni mfumo huo.

"Ukitaka kujua mauzo ya siku, bidhaa ipi inatoka zaidi, kumbukumbu za wateja wako, hasara na mambo yote yanayohusiana na mwenendo wa biashara mfumo wetu wa Buzzyn unakuwezesha," alisema.

Kimaro ametoa rai kwa kampuni, mashirika, wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa kuutumia ili kuwezesha biashara zao kukua na kuendana na kasi ya serikali ya kukuza uchumi.

Mussa alisema mfumo huo unamwezesha mfanyabiashara kujua mwenendo wa biashara yake hata kama yupo mbali nayo.

"Mfumo huu ni wa vijana wazawa tunawaomba watanzania watuunge mkono na unalenga kuweka uhusiano mzuri kati ya mfanyabiashara na mteja wake kwani anayetumia anao uwezo wa kutunza kumbukumbu za wateja na kujua bidhaa zinazofanya vizuri na ambazo hazifanyi vizuri," alisema.




Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akipata maelezo ya ubora wa bidhaa za mvinyo kutoka kwa Mèneja Mauzo wa TDL, Mwesige Mchuruza, alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maonyesho ya Dodoma Wine Festival jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge, TCCIA kushirikiana kuchochea ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameihakikishia Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira itafanya kazi kwa karibu na chemba hiyo ili kutoa mchango stahiki kuchochea ukuaji wa sekta za viwanda, biashara na kilimo.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa ofisi ndogo ya TCCIA Makao Mkuu Dodoma ambapo alimwakilisha Spika Job Ndugai, Dk. Tulia alisema chemba ina nafasi kubwa ya kutoa mchango chanya katika kukuza uchumi wa taifa na kamati ya Bunge itatoa ushirikiano mkubwa.

"Sisi kama Bunge kupitia Kamati yetu ya kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira tupo tayari kushirikiana na TCCIA ilikutoa mchango chanya katika kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Dk. Tulia.

Dk. Tulia ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, aliipongeza TCCIA kwa kuwa mstari wa mbele kuunga mkono jitihada na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali ikiwamo ujenzi wa uchumi unaotegemea viwanda.

"Uzinduzi wa ofisi hii Jiji la Dodoma ambako ndiyo Makao Makuu ya nchi inaonyesha utayari wa sekta binafsi kufanya kazi kwa karibu na serikali. TCCIA ni miongoni wa taasisi za kwanza kwenye sekta binafsi kufungua ofisi hapa," alisema.

Alisema kuwapo kwa ofisi ya chemba Dodoma kutawezesha ushiriki wake kikamilifu kwenye majadiliano na Kamati mbalimbali za Bunge hivyo kusaidia kufanya maamuzi sahihi yatakayo chochea ongezeko na ukuaji wa uwekezaji.

Dk. Tulia alisema amevutiwa na utendaji kazi wa chemba hiyo, kwani imekuwa mstari wa mbele kuwawezesha sambamba na kuwapa huduma za ushauri wa namna bora ya kukuza biashara zao wajasiriamali wanawake vijana (Young Women Entrepreneurs-YWE).

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema uamuzi wa kufungua ofisi hiyo jijini Dodoma unalenga kupunguza gharama wanazozitumia wanachama wake pamoja na wadau wengine kufuata huduma Dar es Salaam.

"Tumeamua kujitanua zaidi kwa kusogeza huduma karibu na wafanyabiashara wenye viwanda, biashara na kilimo kwani uwapo wa ofisi ndogo ya makao makuu kanda ya kati itashughulikia changamoto zote zinazowakabili wanachama wetu kwa haraka," alisema Koyi.

Naye Mjumbe wa Bodi ya TCCIA, Dk. Said Mtemi Kingu, alisema chemba imejimbanua kwa kutekeleza kwa vitendo azma ya serikali ya kujenga uchumi unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025.

# Neema ya maji yatua Chalinze

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imekamilisha utekelezaji wa mradi wa Maji Mlandizi - Chalinze - Mboga wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni tisa zitakazoondoa changamoto ya upatikanaji majisafi kwa mji wa Chalinze iliyodumu kwa muda mrefu.

Aidha, mahitaji halisi ya maji kwa mji wa Chalinze ni lita milioni 12 na kwamba mtambo wa kuzalisha maji wa Wami kwa sasa unazalisha lita milioni 6.8, na kwamba maji yaliyopo yanaweza kuhudumia mji huo kwa miaka miwili ijayo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo na kufungua valvu ili kuruhusu maji kutoka kwenye mtambo kwenda kwa wananchi mwishoni mwa wiki, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema kukamilika kwa mradi wa maji huo kutatoa suluhisho la ukosefu wa maji kwenye maeneo yenye changamoto kwa sasa.

"Serikali inafahamu tabu mnayopitia watu wa Chalinze na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan amehimiza kwa nguvu zote mradi huu ulioasisiwa na aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli ukamilike kwa wakati ili wananchi waweze kupata majisafi, niwapongeze sana DAWASA kwa kazi kubwa mliyoifanya ya kutekeleza mradi huu kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa," alisema Aweso na kuongeza kuwa;

"Niwaombe DAWASA kuhakikisha wananchi wanaunganishwa na huduma ndani ya muda ili jitihada hizi ziweze kuwa na manufaa kwao. Leo tumeweka alama kubwa ya kukamilika kwa mradi huu mkubwa wa Chalinze, hivyo niwatake wananchi kujitokeza kwa ajili ya kupata maunganisho ya maji kwa kufuata taratibu sahihi, pia watendaji watoe ushirikiano mzuri kwa wateja na waunganishiwe ndani ya siku 14," alisema.

Aweso alisema wananchi wakae mkao wa 'kula' kwa kupata huduma ya majisafi kwani tayari amewasha mtambo wa kusukuma maji na kwamba katika ngazi ya kuhakikisha huduma hiyo inawafikia wananchi, serikali iko tayari kusaidia pale DAWASA itakapokwama kwa lengo la kuweza kuwapatia wananchi majisafi na salama.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi wa maji wa Ruvu Juu hadi Mboga utaondoa kero ya upatikanaji wa maji maeneo ya Mlandizi, Chalinze na Mji Mdogo wa Mboga.

Alisema mradi huo unalaza mabomba ya inchi 12 kwa umbali wa kilomita 59 kutoka mtambo ya Ruvu Juu hadi Chalinze, Mji wa Mboga.

Aidha, alisema kiasi cha Sh. bilioni 18 kimetumika mradi wa Maji wa Ruvu Juu mpaka Msoga itakayotatua kero ya maji kwa wananchi zaidi ya 122,000 wa maeneo hayo, na kwamba mradi huo utapeleka maji maeneo ya mji wa Chalinze, Pingo, Pera, Msoga, Bwilingu, Msata, Kihangaiko, na Ubenazimozi.

Awali, Kunenge, alisema Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari; "Mkoa wa Pwani ni mkoa wa kimkakati wa viwanda hivyo ni muhimu kwa wananchi na wawekezaji kuwa na uhakika wa nishati ya umeme na maji yanayotoka kwa uhakika."

Naye Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliishukuru serikali kwa kukamilisha mradi huo kwa kuwa umeleta ahuni kwa wananchi na sasa watatumia muda mwingi kwenye shughuli za uzalishaji.



Mkuu wa Kitengo cha Bia wa Kampuni ya Serengeti (SBL), Nandy Mwiyombella (kulia) na Katibu wa Chama cha MaDJ nchini, Asanterabi Mtaki (kushoto), wakimkabidhi tuzo ya ushindi wa kwanza wa shindano la DJ compeer, Take a Bite Out of Life, Abdulaziz Juma maarufu Dj Dully Tz kutoka Dodoma, ambaye pia alipata seti ya vyombo vya muziki wa uDJ vyenye thamani ya Sh. milioni 7 kutoka kampuni ya SBL. Shindano hilo lililowashirikisha wachezesha muziki zaidi ya 5,200 kote nchini na fainali zake zilifanyika jijini Arusha usiku Jumapili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu Moro yaahidi kuondoa vikwazo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Morogoro, imeahidi kuondoa mambo yanayokwaza jamii na viongozi wa mihimili ya dola ambao wanaona mahali pa kutolea haki pamejaa ufisadi na rushwa, utapeli na lugha za njoo kesho zinazosababisha mateso kwa jamii.

Ahadi hiyo ilitolewa hivi karibuni na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Jaji Paul Ngwembe, katika mkutano wa kwanza uliohusisha wadau wote wa mahakama na viongozi wa serikali katika siku ya kwanza ya kuanza kwa shughuli zake baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan mapema mwezi uliopita. Alisema mambo hayo yanayokwaza jamii pamoja na viongozi wa mihimili ya dola kwa sasa katika mahakama zote za Mkoa wa Morogoro hayataweza kuvumilika ikiwamo kwa watumishi wa mahakama wa ngazi zote.

Kwa mujibu wa Jaji Ngwembe, katika kuhakikisha haki inatolewa kwa wakati wadau wengine ni lazima wabadilike na hawataweza kuvumuliwa ni pamoja Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzui na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Magereza, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), mawakili wa kujitegemea na yeyote anayehusika na haki ya wananchi. Alisema Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro, imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwamo kumaliza mrundikano wa mahabusu magerezani na kwamba taarifa zilizopo Gereza la Morogoro mjini lenye uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 218, lakini hadi Oktoba 11, mwaka huu, walikuwapo wafungwa na mahabusu 560.

"Hii siyo sawa hata kidogo, wajumbe wa kikao hiki ni lazima tuje na mujibu ya kumaliza mrundikano wa mahabusu magerezani kuna mahali hapajakaa sawa katika kazi zetu," alisema Jaji Ngwembe. Alisema mkakati mwingine watakaoshughulikia ni pamoja na ucheleweshwaji wa mashauri mahakamani akieleza kwa kushirikiana na wahusika atahakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa haraka na kuwataka wahusika kubadilika.

"Baada ya kupokea taarifa ya magereza nilimwagiza msajili wa mahakama anipe taarifa ya mashauri ya muda mrefu na mfupi katika ngazi zote za mahakama majibu niliyopata ni mengi, lakini nilistushwa katika taarifa ya Gereza la Morogoro mjini ipo kesi moja mauaji ya mwaka 2012 hadi leo haijasikilizwa," alisema Jaji Ngwembe. Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigella, alisema kuwa kuanzishwa kwa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro kumesaidia kupunguza gharama kwa wananchi kutoka wilaya zote ambao walikuwa wakilazimika kusafiri hadi Dar es Salaam kwenda kupata huduma Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

"Hii itatusaidia sana kupunguza adha walikuwa wakipata wananchi wetu, kuna watu walikuwa wanatoka wilaya ya Malinyi karibu kilometa 400 mpaka Dar es Salaam wanakwenda Mahakama Kuu kusikiliza kesi zao ilikuwa ni gharama kubwa sana, lakini sasa wataishia hapa Morogoro mjini," alisema Shigella.

# Wazawadiwa ufaulu bora darasa la saba

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

UONGOZI wa Shule ya Msingi St. Mathw's iliyoko Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, umewakabidhi vyeti vya ubora vya kitaifa ikiwamo na zawadi wanafunzi wake 42 waliofaulu mitihani yao ya darasa la saba iliyofanyika mwaka huu.

Shule hiyo ilishika nafasi ya kwanza katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani. Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Peter Mutembei, alisema kuwa, katika Wilaya ya Mkuranga shule 76 za msingi zilifanya mitihani ya darasa la saba ambapo shule yao imeshika nafasi ya kwanza kiwilaya.

"Shule za msingi zipo 76 shule yetu imeshika nafasi ya kwanza, katika mkoa shule zikizofanywa mtihani za msingi ni 336, shule yetu imekuwa ya sita na kitaifa shule yetu imekuwa ya 86," alisema.

Aliongeza kuwa wanafunzi wao 40 wamepata ufaulu wa Alana 'A' katika masomo yote huko wanafunzi wawili wakiwa na ufaulu wa alama 'B'.

Alisema mambo sita yakichangia kupatikana kwa matokeo hayo mazuri ni kumtanguliza Mungu, uongozi imara, walimu bora, nidhamu kwa darasa la saba, wazazi kutoa ushirikiano mkubwa ikiwamo kulipa ada kwa wakati na big results now.

Alipongeza serikali kwa kuibua kiwango cha elimu hapa nchini, ikiwamo shule kongwe kuzirudisha katika hali yake ya zamani.

# DC aagiza mifugo inayoharibu mazao kushughulikiwa

**Na Julieth Mkireri,** RUVU

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Abdallah ameagiza uongozi wa Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) kutoa msimamo wa namna ya kukabiliana na mifugo inayoharibu mashamba yao kupitia mkutano mkuu wa chama hicho.

Zainabu alitoa maelekezo hayo juzi alipokuwa akizungumza na baadhi ya wanachama wa CHAURU Ruvu Kata ya Vigwaza Wilaya ya Bagamoyo, na kwamba chama hicho kinatakiwa kuwa na maazimio yake katika kukabiliana na uharibifu wa miundombinu ya shamba hilo ambayo imekuwa ikiharibiwa mara kwa mara na mifugo.

"Wekeni utaratibu kupitia mkutano mkuu wa chama, yeyote anayeingiza mifugo bila kuangalia nafasi yake achukuliwe hatua, wapo watu wanaoshiriki kuwaleta wafugaji kwenye hili shamba wanatakiwa kuwekwa wazi ikiwezekana wachukuliwe hatua," alisema.

Mwenyekiti wa CHAURU, Sadala Chacha, aliomba uongozi wa Wilaya ya Bagamoyo kuingilia kati suala la mifugo kulishwa katika skimu ya umwagiliaji ya mashamba ya chama hicho.

Nipashe Spotika




MAKIPA 10 WALIOOKOA PENALTI NYINGI ZAIDI EPL UK. 12 - 13



# SABABU 5 KWA NINI XAVI ATAFANIKIWA BARCELONA

## ISIKUPITE

HADI kufikia raundi ya tano ya Ligi Kuu Bara, jumla ya wachezaji wanane tayari wameonyeshwa kadi nyekundu; Abdulaziz Makame (Namungu FC), Juma Ramadhani (Polisi Tanzania), Ismail Gambo (KMC FC), Benedictor Jacob (Coastal Union), Anuary Jabir (Dodoma Jiji), Joseph Majagi (Mbeya Kwanza), Santos Mazengo (Ruvu Shooting) na Henock Inonga (Simba).



**BARCELONA,** Hispania

BAADA ya kutimuliwa kwa Ronald Koeman bila kutarajiwa, gwiji wa zamani wa Barcelona, Xavi anatarajiwa kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa klabu hiyo.

Leo Jumatatu klabu hiyo inatarajia kumtangaza rasmi Xavi mwenye umri wa miaka 41, kuwa kocha mpya wa klabu hiyo.

Makala haya yanaangalia sababu tano kwa nini Xavi anaweza kufanikiwa kama kocha mpya wa Barcelona, twende sasa...

### #5. KUFAHAMIANA NA WACHEZAJI WAKONGWE

Baada ya kuondoka katika klabu yake ya utotoni mwaka 2015, Xavi anarejea Catalunya miaka sita. Wakati wake, Barcelona walikuwa kwenye kilele cha ubora wao, wakishinda kila taji akiwa na wachezaji bora zaidi duniani.

Misimu sita baadaye ni wachezaji wanne pekee bado wapo kwenye kikosi hicho ambacho kiliwafunga Juventus na kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Cha kufurahisha ni kwamba wanaunda msingi wa timu ya sasa ya Barcelona, bado wanategemewa licha ya umri wao kuwatupa mkono.

Akiwa amecheza pamoja na Marc-Andre ter Stegen, Sergio Busquets, Jordi Alba na Gerard Pique, Xavi anajua vya kutosha namna ya kufanya nao kazi. Uzoefu wake na wakongwe wa sasa wa Barcelona hakika utamsaidia, kwani 'Blaugrana' hao wanahitaji sana kuhama kutoka kizazi chao cha zamani hadi kingine.

### #4. ALIZALIWA KIONGOZI, UJUZI

Tangu kuhitimu kutoka taasisi ya kifahari ya La Masia, Xavi alianza kuonyesha nia kubwa ya kuongoza upande wake. Kiungo huyo mahiri mara nyingi aliamuru uchezaji wa timu yake, akitumia baadhi ya pasi nzuri kuwahi kuonekana kutoka katikati ya uwanja.

Kiungo huyo wa kati alisifika kwa kutafuta na kutumia nafasi, na mpira ulianzia kwake na kupita kwake. Akiwa na kipaji cha ufundi, Xavi alikuwa na uwezo mkubwa uwanjani, akicheza kwa uwezo wake kwa kumiliki mpira katika mazingira magumu.

Kando na fikra zake za akili na ufahamu wa mbinu, gwiji huyo wa Barcelona pia alikuwa na ujuzi wa uongozi katika siku zake za uchezaji. Xavi alitangazwa rasmi kuwa nahodha wa klabu mwaka 2014 baada ya kustaafu kwa Carles Puyol. Kwa akili na kipaji chake, Xavi atakuwa kiongozi bora wa kuirudisha Barcelona kwenye siku zao za utukufu.

### #3. MKUSANYIKO WA VIPAJI

Kama vile Xavi mwenyewe siku zake za nyuma, Barcelona kwa sasa ina kundi la wachezaji wachanga, tayari kuuteka ulimwengu wakati wowote. Hakika wachezaji hao watahitaji mwongozo wa mkongwe mwenye uzoefu ili kupanua mafanikio yao.

Baada ya kuhitimu kutoka La Masia, Xavi anaelewa kikamilifu utendaji kazi wa kila siku wa akademi inayoheshimika ya Barcelona. Atatoa fursa pana kwa wachezaji wanaostahili ili kupata kiwango cha juu.

Kwa kuzingatia idadi ya vijana waliopo Barcelona, 'Blaugrana' hao wana fursa nzuri ya kuwatumia vema Ansu Fati, Gavi, Ronald Araujo na wengineo. Kwa Xavi, Barcelona wanaweza kupata maajabu katika miaka ijayo.

### #2. REKODI YA KUVUTIA AL SADD

Ingawa mazungumzo mengi yanayomhusu Xavi yamethamini ustadi wake wa kimbinu akiwa mchezaji, kocha huyo mwenye umri wa miaka 41, pia ana namba za kushawishi. Baada ya kustaafu soka mwaka wa 2019, Xavi alichukua jukumu la kuiongoza Al Sadd kama kocha mwaka huo huo.

Katika misimu miwili iliyofuata, kikosi hicho cha nchini Qatar kimeshinda mataji saba tofauti, ikiwa ni pamoja na taji la ligi msimu uliopita. Zaidi ya hayo, kiungo huyo wa zamani wa Barcelona ana rekodi ya kushangaza ya kushinda mechi 63 kati ya 95 akiwa na Al Sadd.

Ingawa Ligi ya Qatar Stars si mashindano ya ngazi ya juu sana ya kandanda duniani, yenye uwezo wa kutosha kuamua ubora wa kocha, hata hivyo, ni kazi ya kwanza ya ukocha wa Xavi. Kuweka kiwango cha ushindi cha asilimia 66.32 katika klabu yako ya kwanza, huku ukidumisha tofauti ya mabao ya zaidi ya 139, ni uthibitisho tosha kwamba Xavi yuko tayari kwa kazi ya Barcelona.

### #1. FALSAFA YA BARCELONA

Sababu muhimu ya kuidhinisha uamuzi uliopendekezwa wa kumchagua Xavi kama kocha mkuu wa Barcelona ni historia yake tajiri na klabu hiyo. Ukiondoa mapumziko ya miaka sita akiwa kule Mashariki ya Kati, Mkatalunya huyo ametumia maisha yake yote ya soka, akiwa na mkataba na klabu moja tu, Barcelona.

Mhitimu wa La Masia, Xavi amepata elimu yake ya soka chini ya baadhi ya wataalamu bora wa wakati wote wa Blaugrana hao, akiwamo Pep Guardiola, Louis van Gaal na Luis Enrique. Kwa hiyo, gwiji huyo wa Hispania si mgeni katika falsafa ya Barcelona; itikadi ambayo imepotea njia pale Camp Nou katika miaka ya hivi karibuni.

Huku Rais Joan Laporta akijaribu kadri awezavyo kurudisha kiburi cha Barcelona kilichopotea, Xavi anaweza kuwa ndio kiongozi wa ubora huo. Tayari wakiwa na rais mwenye mapenzi na kikosi cha kusisimua na cha vijana, Barcelona wanahitaji tu kocha mahiri aliye na uhusiano mkubwa na klabu ili kuleta mafanikio mapya. Na Xavier Hernandez Creus anatosha kikamilifu.

## Extra Time

# MAKIPA 10 WALIOOKOA PENALTI NYINGI ZAIDI EPL

**LONDON,** England

LIGI Kuu Egland imekuwa ikipambwa na magolikipa wengi bora kwa miaka mingi. Wengi wa makipa hawa wametimiza majukumu yao muhimu katika timu zilizoshinda mataji. Makipa wawili kama hao wa sasa ni Alisson wa Liverpool na Ederson wa Manchester City.

**Ingawa ni makipa bora kwa kiwango chao wenyewe, lakini si miongoni mwa waokoaji bora wa penalti katika historia ya Ligi Kuu England. Hiyo ni kwa sababu timu zao zote zina ulinzi mkali ambao hauruhusu penalti nyingi.**

Hiyo inatuleta kwenye kile kinachohitajika kuokoa penalti kwani kipa ana uwezekano wa kuanza. Kwa kuzingatia kasi ya mpira kutoka yadi 12, kikomo cha muda wa athari ya binadamu inamaanisha walinda mlango hawawezi kusubiri kuona mpira kutoka kwa mguu wa mpiga penalti kabla ya kuchagua mwelekeo wa kupiga mbizi. Lakini makipa wa juu huokoa penalti nyingi. Wanafanyaje hivyo?

Naam, wanasimama kidete kwa kuchelewa iwezekanavyo, wanashinda akili dhidi ya mpiga penalti. Michezo ya goli inaweza pia kumvuruga mpiga penalti. Lakini makipa wengi wanajua ni njia gani mpiga penalti huwa anapiga penalti yake; kwa hivyo wanapiga mbizi (au hawafanyi) ipasavyo.

Kwa maelezo hayo, hapa tunawaangalia magolikipa 10 katika historia ya Ligi Kuu England waliookoa penalti nyingi zaidi, haya sasa...

Kumbuka: Takwimu zote ni kwa mujibu wa premierleague.com isipokuwa kama zimetajwa vinginevyo.

### #10. BRAD FRIEDEL - 6

Brad Friedel alikuwa na kazi ndefu na nzuri kwenye Ligi Kuu, akicheza mechi 450 katika klabu nne tofauti.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Marekani aliokoa penalti sita katika maisha yake ya takriban miongo miwili. Friedel ni mmoja wa makipa wachache wa Ligi Kuu waliofunga mabao.

Ni mmoja wa makipa watatu waliookoa penalti nne katika msimu wa Ligi Kuu 2006-07.

Penalti ya mwisho ya Friedel kuokoa kwenye Ligi Kuu ilipigwa na Dean Whitehead msimu wa 2007-08.

### #9. MANUEL ALMUNIA - 6

Manuel Almunia alifurahia muda mfupi, lakini mzuri kwenye Ligi Kuu akiwa na Arsenal katika miaka ya 2000 na mwanzoni mwa 2010.

Raia huyo wa Hispania alicheza zaidi ya michezo 100 kwenye ligi na 44 bila kuruhusu bao. Ingawa hakushinda taji la Ligi Kuu akiwa na klabu hiyo, Almunia alijipatia umaarufu pale Emirates kwa kuokoa mikwaju yake ya penalti. Aliokoa penalti tano kati ya sita.

Almunia aliokoa penalti nyingi za Ligi Kuu katika misimu miwili tofauti. Penalti yake ya mwisho kuokoa kwenye ligi ilikuwa ya Chris Brunt msimu wa 2010-11.

### #8. JUSSI JAASKELAINEN - 7

Jurri Jaaskelainen alikuwa na nafasi nzuri ya muongo mmoja na nusu katika Ligi Kuu miaka ya 2000 na mwanzoni mwa 2010.

Kipa huyu wa kimataifa wa Finland alicheza mechi 436 katika klabu mbili tofauti, huku akiwa amecheza mechi 100 bila kuruhusu bao. Mengi ya penalti alizoziokoa zilikuja katika kipindi cha muongo mmoja akiwa Bolton Wanderers.

Ingawa hakushinda taji la Ligi Kuu, lakini alijijenga kama mmoja wa waokoaji wazuri wa penalti.

Jaaskelainen aliokoa penalti kutoka kwa wachezaji kama Ruud van Nistelrooy na James Milner kwenye Ligi Kuu. Penalti yake ya mwisho kuokoa ilikuwa ni ya Ashley Young msimu wa 2010-11.

### #7. TIM HOWARD - 7

Tim Howard ni mmoja wa makipa mashuhuri wasio Waingereza katika historia ya Ligi Kuu.

Mmarekani huyo alicheza takribani michezo 400 katika mashindano hayo kwa klabu tatu tofauti, huku akicheza mechi 132 bila kuruhusu bao. Mmoja wa makipa bora ambaye hajashinda taji la Ligi Kuu, Howard alikuwa kielelezo cha uthabiti wakati akiwa pale Everton.

Bila kustaajabisha, aliokoa penalti wakati wa maisha yake ya Ligi Kuu, akiokoa tatu kati ya hizo msimu wa 2011-12.



HEURELHO GOMES

Howard aliokoa penalti kutoka kwa wachezaji kama Dirk Kuyt, Sergio Aguero na Christian Benteke kwenye Ligi Kuu. Mara yake ya mwisho kuokoa penalti kwenye ligi hiyo ilikuwa ni ya Daniel Sturridge msimu wa 2013-14.

### #6. JOE HART - 7

Joe Hart amekuwa na mafanikio kwenye Ligi Kuu. Mwingereza huyo amecheza takriban mechi 350 kwenye ligi hiyo katika klabu nne tofauti.

Sasa akiwa Celtic, kipa huyo mwenye umri wa miaka 34, alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu, yote akiwa na Manchester City. Hart pia alicheza mechi 10 bila kuruhusu bao katika kipindi cha misimu saba mfululizo.

Katika hali ya kushangaza, penalti tano kati ya saba alizookoa kwenye ligi zilikuja wakati akicheza Man City.

Hart aliokoa penalti za wachezaji kama Frank Lampard na Wayne Rooney kwenye Ligi Kuu. Penalti yake ya mwisho kuokoa ilikuwa ni ya Paul Pogba msimu wa 2018-19 alipokuwa akiichezea Burnley.

### #5. LUKASZ FABIANSKI - 7

Lukasz Fabianski ni mmoja wa makipa wachache kwenye orodha hii ambao bado wapo kwenye Ligi Kuu England.

Kipa huyo wa kimataifa wa Poland, amecheza takriban mechi 300 kwenye ligi hiyo kwa klabu tatu tofauti, huku nyingi zaidi akiwa Swansea City. Ingawa alianza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2007-08 akiwa na Arsenal, ilikuwa ni karibu muongo mmoja baadaye (2016-17) alipookoa penalti yake ya kwanza kwenye mashindano hayo.

Tangu wakati huo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ameokoa penalti sita zaidi katika Ligi Kuu England.

Kipa huyo wa West Ham alizuia penalti mbili kwenye Ligi Kuu msimu uliopita.

### #4. SIMON MIGNOLET - 8

Simon Mignolet alifurahia mafanikio yaliyodumu kwa takriban muongo mmoja kwenye Ligi Kuu. Alicheza takriban mechi 250 kwenye ligi hiyo akiwa na klabu mbili tofauti, huku akiwa hajaruhusu bao kwenye mechi 80, nyingi akiwa na Liverpool.

Akiwa pale Anfield kipa huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ndipo alipotengeneza sifa yake kama mwokoaji mzuri wa penalti. Ingawa hakuwa katika timu ya Liverpool iliyoshinda Ligi Kuu msimu wa 2019-20, Mignolet amekuwa na kipindi cha mafanikio katika mashindano hayo.

Mignolet penalti yake ya mwisho ya Ligi Kuu kuokoa ni ile ya Jamie Vardy wa Leicester City msimu wa 2017-18, mchezo ambao Liverpool walishinda 3-2.

### #3. BEN FOSTER - 8

Ben Foster alionekana kama angekuwa kipa bora zaidi kwenye Ligi Kuu wakati alipowasili pale Manchester United msimu wa 2007-08.

Muongo mmoja na nusu baadaye, Foster alishindwa kukidhi matarajio. Hata hivyo, mlinda mlango huyo wa Watford amekuwa na msimu mzuri wa Ligi Kuu England, akiwa amecheza mechi 83 bila kuruhsu bao kwenye michezo 369 kwa klabu nne tofauti.

Pamoja na yote, Foster pia amejijengea sifa ya kuokoa penalti. Penalti zake nyingi alizookoa akiwa na West Bromwich Albion.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka miaka 38, penalti yake ya mwisho ya Ligi Kuu kuokoa ilikuwa ni ile ya Raheem Sterling wa Manchester City msimu wa 2019-20.

### #2. ROBERT GREEN - 9

Robert Green alikuwa na maisha bora kwenye Ligi Kuu. Alicheza zaidi ya mechi 250 katika mashindano hayo kwa klabu nne tofauti na kucheza mechi 53 bila kuruhusu bao.

Green, ingawa, ni mmoja wa wazuiaji wa penalti waliofaulu zaidi katika historia ya Ligi Kuu Ni mmoja kati ya makipa wawili waliookoa penalti tisa kwenye Ligi Kuu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 41, amewanyima penalti wachezaji kama Cristiano Ronaldo, Alexis Sanchez na Steven Gerrard (mara mbili). Kwa kweli, kuokoa penalti yake ya mwisho kwenye mashindano hayo ilikuwa ni ile ya Gerard msimu wa 2014-15, alipokuwa akiichezea Queens Park Rangers.

### #1. HEURELHO GOMES - 9

Heurelho Gomes alicheza takriban mechi 200 kwenye Ligi Kuu katika klabu mbili tofauti, Tottenham Hotspur na Watford.

Mbrazil huyo, ambaye amecheza mechi 50 za Ligi Kuu bila kuruhusu bao, ni mmoja wa makipa bora wawili tu katika historia ya ligi kuokoa penalti tisa. Gomes, kwa kweli, ndiye kipa wa kwanza kwenye Ligi Kuu kuokoa penalti nyingi angalau katika mechi mbili.

Alifanya hivyo kwa Spurs dhidi ya Sunderland msimu wa 2009-10, kabla ya kurudia akiwa na Watford dhidi ya West Bromwich Albion msimu wa 2015-16. Mara zote mbili, aliwanyima wapigaji wale wale mara mbili - Darren Bent (Sunderland) na Saido Berahino (West Bromwich Albion). Kwa kweli, Gomes amemnyima Bent penalti mara tatu.


Penatli ya mwisho kuokolewa na Mbrazil huyo kwenye ligi hiyo ilikuwa ni ya Christian Benteke wa Crystal Palace msimu wa 2015-16.

## Nukuu

"Kitu pekee wanachokosa kwenye chumba cha kubadilishia nguo ni kocha mwenye uzoefu. Ingawa makocha hao ni wazuri, hawajapata uzoefu kwa sababu bado hawajafikia umri wa kutosha. Kazi kuu ya Mick Phelan (Kocha Msaidizi wa United) sio kufundisha kila siku. Labda aliifundisha timu yetu mara kadhaa. Ana sifa zingine ambazo ni bora. Sir Alex [Ferguson] kila mara alikuwa bingwa Mick Phelan." **Beki nguli wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, akimkosoa Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer baada ya kipigo dhidi ya City juzi.**



"Haikuwa kwaheri, ilikuwa 'kuonana hivi karibuni' Camp Nou imekuwa nyumbani kwangu kila wakati. Ninyi ni mashabiki wangu, watu wangu, klabu ninayoipenda zaidi. Na sasa, narudi nyumbani. Tutaonana hivi karibuni," **Kocha mpya wa Barca anayetarajiwa kutambulishwa rasmi leo, Xavi.**



"Ninauhakika kwamba msimu huu mtaona ubora wake na atacheza zaidi kuliko anavyofanya sasa. Hazard [Eden] analo hilo. Kila kitu: ubora, hamasa. Kinachotokea mara nyingine kocha anapenda kutoa nafasi kwa wachezaji wengine," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti akimzungumzia Eden Hazard.**





Straika wa Simba, Kibu Denis, akipiga hesabu za kumlamba chenga mchezaji wa Namungo, Abdulmalik Zacharia, kwenye mechi ya raundi ya tano ya Ligi Kuu, Uwanja wa Benjamin Mkapa. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MAKTABA**

# KADI NYEKUNDU, SARE, ZATIKISA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imemaliza raundi tano ikishuhudia idadi kubwa ya mechi za sare, huku raundi hiyo pekee ikiwa na sare nne. Pia kumekuwa na idadi kubwa ya kadi, zikiwamo nyekundu kwenye mechi za hivi karibuni, huku Uwanja wa Benjamin Mkapa ukizalisha kadi nyekundu sita, Simba na Yanga zilipocheza dhidi ya wapinzani wao.

Kwa mujibu wa takwimu zetu ni kwamba jumla ya michezo 40 imeshachezwa, kukiwa na sare 16 mpaka sasa, nne zikipatikana kwenye raundi ya tano. Aidha, mechi 24 zimetoa mshindi, 16 zikiwa sare, hivyo kuwa na tofauti ya mechi nane tu kati ya ushindi na sare.

Sare nne za hivi karibuni ni za Simba ikilazimishwa suluhu dhidi ya Coastal Union Jumapili iliyopita, Mbeya Kwanza ikienda sare ya mabao 2-2 dhidi ya Polisi Tanzania, Jumatatu iliyopita, wakati Coastal Union ililazimishwa tena suluhu ya bila kufungana dhidi ya Prisons, Jumatano iliyopita na siku hiyo hiyo, Biashara United ikatoka suluhu dhidi ya Mbeya City.

Tayari kulikuwa na sare 12, kabla ya mechi hizo za raundi ya tano ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## KADI NYEKUNDU KAMA NJUGU

Katika mechi tatu mfululizo zilizochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kadi nyekundu nne zimepatikana michezo tofauti, huku mbili zikiwa kwenye mechi moja.

Kwenye mechi ya Jumatano iliyopita kati ya Simba na Namungo, mchezaji Abdulaziz Makame alilimwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Shomari Kapombe, mechi ambayo ilimalizika kwa Simba kushinda bao 1-0.

Kabla ya mechi hiyo, Jumanne iliyopita, beki wa Ruvu Shooting, Santos Mazengo alizawadiwa kadi nyekundu kwa kumchezea madhambi straika wa Yanga, Fiston Mayele, mechi ambayo ilimalizika kwa Yanga kushinda mabao 3-1 uwanja huo huo wa Mkapa.

Jumapili ya Oktoba 31 kwenye uwanja huo kulikuwa na mechi Simba ikicheza dhidi ya Coastal zikitoka sare bila kufungana, lakini wachezaji wa timu zote mbili, Benedict Jacob wa Coastal na Enock Inonga wa Simba walionyeshwa kadi nyekundu kwa makosa tofauti kila mmoja.

## MECHI ZA SIMBA KAMA VITA

Mechi za Simba ndizo zinazoonekana kuwa na kadi nyingi nyekundu. Kati ya mechi tano ambazo imecheza, ni mechi moja tu ambayo haikuwa na kadi nyekundu, huku kwenye michezo minne ambayo imecheza ikizaliwa kadi tano nyekundu.

Mechi ya kwanza dhidi ya Biashara United ndiyo haikuwa na kadi, lakini hali ilianza kubadilika kwenye mechi dhidi ya Dodoma Jiji, mchezaji Anuary Jabir alipotolewa kwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Kennedy Juma na kwenye mechi iliyofuata dhidi ya Polisi Tanzania, Juma Ramadhani alilimwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya, Bernard Morrison.

Baada ya hapo ilifuata mechi dhidi ya Coastal Union, ambapo mbali ya wapinzani wao kupata kadi nyekundu, ikitolewa kwa Benedict Jacob, Henock Inonga naye alipata kadi kama hiyo.

Kadi nyekundu nyingine kwenye mechi ya Simba, ilipatikana ikicheza dhidi ya Namungo baada ya Abdulaziz Makame kutwangwa kadi hiyo, baada ya kumchezea rafu Shomari Kapombe.

## REKODI YA DIARRA YAVUNJWA

Licha ya ushindi wa mabao 3-1 Jumanne iliyopita dhidi ya Ruvu Shooting, rekodi ya kipa wa Yanga Djigui Diarra ya kutoruhusu nyavu zake kuguswa, imevunjwa baada ya kutunguliwa bao dakika ya nane tu na Shaaban Msala wa Ruvu Shooting.

Kabla ya hapo, kipa huyo raia wa Mali alikuwa amecheza mechi nne bila wavu wake kuguswa.

## MANULA AENDELEA KUPETA

Kipa wa Simba, Aishi Manula ameendelea kulinda rekodi yake ya kutoruhusu bao kwenye lango lake hadi kufikia raundi ya tano ya Ligi Kuu.

Manula, amefikisha mechi tano akisimama golini na kutoruhusu bao. Wakati Diarra wa Yanga alifungwa kwenye mechi ya raundi ya tano timu yake ikishinda mabao 3-1, Manula ambaye kwenye mechi ya raundi hiyo timu yake ilicheza dhidi ya Namungo, hakuruhusu bao huku timu yake ikishinda bao 1-0.

## MBEYA KWANZA WABAYA MWISHONI

Timu ya Mbeya Kwanza imeonyesha kuwa na uwezo wa kurudisha mabao kipindi cha pili, hivyo timu zinazocheza nayo, zisijiamini zinapokuwa mbele hata kwa mabao mengi.

Mara tatu kwenye raundi tano, imekuwa ikitoka nyuma na kurudisha mabao.

Jumatatu iliyopita, ikiwa nyuma kwa mabao 2-0 dhidi ya Polisi Tanzania, ilirudisha yote na mechi ikaisha kwa mabao 2-2.

Haikuwa mechi hiyo tu, Oktoba 3, ilirudisha mabao yote mawili na kwenda sare ya 2-2 dhidi ya ndugu zao Mbeya City.

Oktoba 29, pia ilirudisha bao dakika tisa kabla mechi kumalizika, ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Biashara United.

## NAMUNGO INAFUNGWA USIKU

Ukiachilia mbali kuwa ni kweli mechi mbili ambazo Namungo imefungwa dhidi ya Azam FC na Simba zilichezwa usiku, lakini imekuwa ikiruhusu mabao dakika za mwisho.

Jumatano iliyopita Uwanja wa Benjamin Mpaka, iliruhusu kufungwa bao 1-0 likiwekwa wavuni na Meddie Kagere kwenye dakika nne za nyongeza, lakini ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wao wa Chamazi, Oktoba 19 kwa mbao la dakika ya 90 lililofungwa na Idriss Mbombo.

## JE, WAJUA?

NBC PREMIER LEAGUE

HADI wakati huu Ligi Kuu Bara ikiwa imefikia raundi ya tano timu ya Polisi Tanzania ndiyo kinara wa kadi baada ya wachezaji wake kuzawadia kadi za njano 14 na nyekundu moja ikifuatiwa na KMC FC (njano 12, nyekundu 1) huku Mbeya City ikifuata kwa njano 10. Yanga ndiyo timu yenye idadi ndogo zaidi ya kadi (njano 2) ikifuatiwa na Simba (njano 4 na nyekundu 1).

na familia zao.







# Mabadiliko kiutendaji kufanyika TBS, WMA

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WIZARA ya Viwanda na Biashara inatarajia kufanya mabadiliko ya kiutendaji kwa taasisi mbili ambazo ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo nchini (WMA) kutokana na kuwa na mwingiliano wa majukumu.

Sambamba na hilo, yatafanya mapitio ya sera mbili zinazosimamia wizara hiyo hususani eneo la viwanda.

Waziri wa Wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alitoa kauli hiyo jijini hapa juzi alipokuwa akifungua kikao kazi cha taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo.

Alisema ili kuhakikisha kuna ufanisi ndani ya wizara wanakusudia kuangalia muundo wa taasisi hizo ili kufanya mabadiliko au zifanye kazi moja.

"Tutaangalia kama tuhamishe taasisi moja kwenda kwenye nyingine au majukumu yabaki kwa mmoja au zifanye kazi kwa pamoja hivyo nikaona niwashirikishe kwanza," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa wanakusudia kufanyia mapitio ya sera ya maendeleo ya viwanda na tayari mapendekezo ya sera mpya yameandaliwa, lakini lazima wadau washirikishwe ili kujadili kwa pamoja kabla ya kufanya uamuzi.

Prof. Mkumbo alisema wataanza kupima mafanikio ya kiutendaji kwa kutengeneza mikataba ili kujua kila taasisi inawajibika vipi na kama haijawajibika inavyotakiwa mabadiliko yafanyike.

"Kwa sasa wizara ina changamoto ya kanzidata ya taarifa na takwimu lengo likiwa ni kufahamu taasisi fulani imefanya nini na imezalisha kwa kiasi gani, Mfano hapa ukimuuliza Mkurugenzi wa Tantrade kuna biashara ngapi hajui, ataanza kukuna kichwa, lakini lazima tuwe na Annual Report ya viwanda maana bila kuwa na takwimu hatuwezi kufanya maamuzi sahihi," alisema.

Alibainisha kuwa viwanda vipo, lakini tatizo lililoko ni kuwa vyote ni vidogo, hivyo waangalie namna ya kuvikuza na kuviongeza.

# Mchumi nguli kuwa mzungumzaji mkuu kongamano utafiti, biashara

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

MCHUMI Mashuhuri wa Kimataifa, Prof. Justin Yifu Lin, anatarajiwa kuwa mzungumzaji mkuu kwenye kongamano la 25 la Utafiti na Biashara kuhusu ushindani wa Viwanda na Biashara linatarajiwa kufanyika Jumatano jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dotto James, alisema Lin ni mwanzilishi wa Taasisi ya Misingi mipya ya uchumi katika Chuo Kikuu cha Peking na amewahi kuwa Mchumi Mkuu wa Benki ya Dunia (WB).

Alisema kongamano hilo linalenga kuchochea na kukuza mijadala ya kisera na utafiti kuhusu viwanda na biashara kama sekta muhimu ya kuharakisha ukuaji uchumi na kichocheo cha mabadiliko ya kimuundo.

James alisema mabadiliko ya muundo wa uchumi muhimu katika kutengeneza ajira zinazohitajika kwa vijana, kupunguza umaskini, na kuimarisha ustahimilivu wa kiuchumi dhidi ya majanga mbalimbali.

"Kongamano hilo limebeba kaulimbiu isemayo Mapinduzi ya Uchumi wa Tanzania kupitia ushindani wa viwanda na biashara ambayo ni muhimu kwani inafungamana vyema na msukumo wa mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano unaosisitiza kuendeleza juhudi za kuleta mageuzi ya uchumi, kuboresha ushindani wa kitaifa kwa maendeleo ya watu," alisema.

Alieleza kuwa kongamano hilo litahudhuriwa na washiriki 200 na litafanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu, Julius Nyerere jijini Dar es Salaam na kufunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

"Viwanda na biashara shindani ndio vichocheo muhimu vya mabadiliko ya kimuundo na ukuaji. Hii inaelezea ushirikiano unaoendelea kati ya wizara ya viwanda na biashara na REPOA kwa warsha hii na programu nyingine za utafiti na kujenga uwezo juu sekta hizi," alisema.

Alisema kongamano hilo linaandaliwa na REPOA na kufanyika kila mwaka huwakutanisha watafiti wabobezi, watunga sera, washiriki wa maendeleo, AZAKI, sekta binafsi na wasomi kutoka taasisi za elimu ya juu nchini na nje ya nchi ili kujadili masuala ya maendeleo, matokeo ya utafiti kutoka kwa watafiti waliobobea ili yasaidie kuboresha sera na kuchangia kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kuboresha maisha ya Watanzania.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema makongamano yaliyofanyika siku za nyuma yameleta mchango mkubwa kwa taifa na sekta ya viwanda na biashara kwa ujumla.




Baadhi ya wakulima wa zao la zabibu mkoani Dodoma wakipata maelezo kwa wataalamu wa kilimo kutoka kituo cha utafiti wa mazao cha TARI Makutupora walipotembelea banda hilo, katika maonyesho ya Dodoma Wine Festival yaliyofanyika mwisho wa wiki kwenye viwanja vya mashujaa jijini Dodoma. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Wenyeviti waagizwa usimamizi wa fedha

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ameundua Umoja wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji Tanzania, huku akiwaagiza kusimamia fedha za miradi ya maendeleo zinazopelekwa katika maeneo yao.

Silinde aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza na viongozi na wajumbe wa umoja huo.

Alisema viongozi hao ndio walengwa katika maeneo wanayoishi na wananchi kwa kuona na kusimamia maendeleo ya miradi inayopelekwa ambayo ni ujenzi wa miundombinu huduma za kiuchumi na kijamii.

"Serikali inatambua mchango na jitihada za Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji nchini zikiwamo pamoja na changamoto," alisema Silinde na kuongeza kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imezitaka halmashauri zote nchini kutoa fedha za ujenzi, kukarabati pamoja na ununuzi wa samani za ofisi hizo ili viongozi hao waweza kutoa huduma bora kwa wananchi. Akizungumzia kuhusu stahiki za viongozi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, Silinde alisema serikali imeweka utaratibu kwa kila mtaa au kijiji kulipa posho kutokana na mapato yao.

"Halmashauri zote nchini hupaswa kurejesha mapato ya Kijiji/Mtaa yanajumuisha mapato yanayotokana na asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya halmashauri nakiri kwamba utekelezaji wake unatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine," alisema.

Aliwaagiza viongozi wa umoja huo kuisaidia serikali katika kushirikiana na watendaji wa mitaa, vijiji na vitongoji kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kuzipa heshima Mamlaka za Serikali za Mitaa lakini kutatua kero za wananchi hasa migogoro ya ardhi nchini kwa kuwa hilo linaanzia kwao.

"Hakikisheni mnaepuka kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi katika maeneo yenu kwa kushiriki kuuza au kushuhudia uuzaji wa ardhi kwa mnunuzi zaidi ya mmoja na bila kuzingatia sheria ikiwamo maeneo ya wazi, maeneo yaliyohifadhiwa au maeneo ya kingo za mito na bahari kinyume na sheria," alisema Silinde.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Lucas Mwasongwe, aliishukuru serikali kwa kutambua mchango wao na kuiomba iendelee kuona umoja huo kwa kuwa wao wana nafasi kubwa kwa jamii katika kuleta maendeleo ya nchi.



# Mbarali wakopeshwa matrekta 241

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

KAMPUNI ya usambazaji wa zana za kilimo ya Agricom Africa kwa kushirikiana na Benki ya CRDB, zimetoa mikopo ya matrekta madogo (power tillers) 241 kwa wakulima wa Wilaya ya Mbarali ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mikopo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Agricom Africa, Alex Duffar, alisema mkopo huo ni mwendelezo wa kampuni hiyo katika kuwasaidia wakulima kupata zana za kisasa za kilimo na kwamba una thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.6 .

Alisema mwaka jana walitoa mkopo wa matrekta kama hayo 161, lakini kutokana na mahitaji ya wakulima kuwa makubwa waliamua kuongeza kiwango na kufikia matrekta hayo 241 ambayo wamekopesha sasa.

"Pamoja na kuwakopesha zana hizi, pia tutatoa mafunzo maalumu kwa wakulima hawa namna ya kuzitumia ili zidumu muda mrefu na ziwasaidie kuleta tija ambayo inakusudiwa, hizi ni mashine za kisasa kabisa," alisema Duffar.

Alisema wamebaini kuwa wakulima wa wilaya hiyo wana mahitaji makubwa ya zana za kisasa za umwagiliaji, hivyo wamepanga kuzileta mwakani na kuwakopesha wakulima ili tija iongezeke zaidi.

Vilevile, alisema kampuni hiyo ina mpango wa kuanzisha mfumo wa stakabadhi gharani ili kuwasaidia wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri ambayo itaendana na gharama za uzalishaji.

Mwakilishi wa Benki ya CRDB, Cornelius Msigwa, alisema benki hiyo imekuwa ikitoa mikopo mingi kwenye sekta ya kilimo hasa katika Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuendeleza mazao mbalimbali ambayo ni ya chakula na biashara.

Alisema katika msimu uliopita, benki hiyo ilitoa mkopo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 150 kwa wakulima wa Wilaya ya Mbarali pekee, na kwamba mbali na wilaya hiyo pia wamekuwa wakitoa mikopo katika wilaya zingine za mkoa huo.

Alisema wamekuwa wakitoa mikopo kwenye kilimo cha tumbaku wilayani Chunya pamoja na kilimo cha chai na maparachichi katika Wilaya ya Rungwe, na kwamba mkopo kwenye maeneo hayo umefikia thamani ya Sh. bilioni 30.

Akipokea na kukabidhi mikopo hiyo kwa wakulima, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliushukuru uongozi wa Agricom pamoja na Benki ya CRDB kwa kutoa mikopo hiyo akidai kuwa itasaidia kuinua kilimo. Homera alisema mkopo huo utawasaidia wakulima kuondokana na matumizi ya zana duni za kilimo ambazo zilikuwa zinawapunguzia ufanisi kwenye uzalishaji wa mpunga.

Aliwataka wakulima hao kuhakikisha wanaongeza uzalishaji ili wawe na uwezo wa kuongeza akiba ya chakula pamoja na kuuza ziada ili wafanye maendeleo mengine.

Aliwahakikishia kuwa soko la mchele kwa sasa ni la uhakika kutokana na mchele wa Tanzania kupata soko nchini Kenya baada ya mazungumzo ya hivi karibuni kati ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyata.

"Sasa hivi kila siku malori zaidi ya 15 yanasafirisha mchele kutoka Mbeya kwenda Nairobi nchini Kenya, sasa nawashauri wakulima mwongeze uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko hilo na muwe na uhakika wa kurejesha mikopo hii," alisema Homera.

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa maeneo nchini yanayozalisha mpunga kwa kiwango kikubwa, lakini tatizo lililokuwa likiwakabili wakulima wa eneo hilo ni kukosa zana za kisasa za kulimia.



Baadhi ya vijana wanaofanya kazi kwenye mashine za kukoboa mpunga zilizoko Soko la Kimataifa la Mchele Kata ya Igurusi, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wakipanga magunia ya mpunga nje ya mashine hizo mwishoni mwa wiki kabla ya kuupeleka mashineni kwa ajili ya kokobolewa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wenye ulemavu wahamasishwa chanjo ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WATU wenye ulemavu wilayani Mbarali, wameshauriwa kujitokeza kuchanja chanjo ya kujikinga na corona kwa maelezo kuwa virusi hivyo vinaua bila kuchagua hali ya viungo vya mtu.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu wa Chama cha watu wenye ulemavu wa wilaya hiyo, Ramadhan Shamte, wakati wa mkutano wa Chama cha Watu wenye Ulemavu Kata ya Igurusi wilayani humo ulioitishwa na Taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya SALIOTA.

Alisema wataalamu wa afya wamethibitisha kwamba chanjo hiyo ni salama na inamfanya mtu aliyechanja kuwa na uwezekano mdogo wa kupata maambukizi na hata akiambukizwa madhara yake yanakuwa madogo kuliko ambaye hajachanjwa.

Shamte alisema kwa sasa kupitia chama chao wanahamasishana ili kila mwanachama achanjwe, na kwamba wanafuata miongozo yote ya serikali ikiwamo kutolazimishana kuchanja na badala yake wanaendelea kutumia utaratibu wa hiari.

"Sisi hatupeani elimu ya corona pekee bali hata magonjwa mengine ya kuambukizwa ukiwamo Ukimwi, magonjwa haya hayachagui mwenye ulemavu wala mzima, hivyo kila mmoja lazima ajihadhari na sisi tunatumia jukwaa letu kupeana elimu," alisema Shamte.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu na kuwahamasisha kuchanja ili wananchi wote wawe salama na shughuli za maendeleo ziendelee kufanyika. Baadhi ya watu wenye ulemavu wa Kata ya Igurusi walisema chanjo hiyo ni muhimu kutokana na kwamba mazingira ya virusi hivyo kuenea hata wao wanakutana nayo ikiwamo mikusanyiko.

Mmoja wa watu wenye ulemavu, Joyce Sanga, alisema ameshachanja, na kwamba aliamua kuchanja kwa ajili ya kuilinda afya yake yeye mwenyewe na familia yake baada ya kuridhika na elimu iliyotolewa na wataalamu.

Alisema kuna baadhi ya watu wanaogopa kuchanja kwa sababu ya maneno ya upotoshaji yanayotolewa na baadhi ya watu wasiokuwa na utaalamu wowote jambo ambalo aliwataka watu wenye ulemavu kuwa makini.

"Hii chanjo isingekuwa salama nina uhakika Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan asingechanja, alitushauri wananchi wote tuchanje kwa ajili ya usalama wa afya zetu wenyewe na nawashauri wenzangu wasisikilize maneno ya wapotoshaji," alisema Joyce.

Mkurugenzi wa Shirika la SALIOTA, Elisha Mwanikawaga, alisema shirika hilo limekuwa likishirikiana na serikali kuhamasisha wananchi kwenye shughuli mbalimbali ikiwamo masuala ya afya.

Alisema moja kati ya majukumu ambayo shirika hilo linafanya kwa sasa ni kuhamasisha makundi mbalimbali ya wananchi kujitokeza kuchanjwa chanjo dhidi ya virusi vya corona, na kwamba ndio maana waliamua kuwakusanya watu wenye ulemavu na kuwapatia elimu hiyo.

Alisema shirika hilo pia linatoa elimu kuhusu maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa kundi hilo, kutokana na kwamba kuwa miongoni mwa makundi ambayo yapo kwenye hatari ya kuambukizwa virusi hivyo.

# Wanawake watakiwa kutovumilia kufanyiwa vitendo vya ukatili kijinsia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE mkoani Mbeya wameshauriwa kutovumilia vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia wanaofanyiwa kwenye jamii, badala yake wanatakiwa kutoa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika.

Amesema kwamba kwa kutoa taarifa, hatua hiyo itasaidia wanaofanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua za kisheria.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na mwanaharakati wa haki za wanawake mkoani humo, Aikande Lema, ambaye ni wakili wa kujitegemea wakati wa mkutano wa Umoja wa Vikundi vya Wanawake wa Mkoa wa Mbeya ujulikanao kwa jina la Familia Moja.

Alisema katika ndoa wanawake wanafundishwa kuwa wavumilivu, lakini sio kila matukio wanatakiwa kuyavumilia kwa maelezo kuwa baadhi ya matukio ya ukatili wanayofanyiwa yanawaathiri kiafya, kiuchumi na kisaikolojia.

Alisema wapo baadhi ya wanawake wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa kijinsia kwenye familia zao, lakini wanavumilia bila kutoa taarifa hali ambayo wakati mwingine inawasababishia madhara.

"Kuna baadhi wanapigwa vipigo ambavyo sio vya kawaida, toeni taarifa kwenye mamlaka msivumilie, mimi najua vizuri sheria, hivyo ukiwa na jambo lolote ambalo linahusu sheria na unataka ufafanuzi niko tayari kuwasaidia," alisema Aikande.

Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye mkutano huo, aliwataka wanawake kujituma kufanya kazi ili kujiletea maendeleo wao wenyewe, familia zao na taifa kwa ujumla.

Mwaselela ambaye ni mwekezaji kwenye sekta ya elimu, alisema wanawake wameonyesha kuwa na uwezo mkubwa kwenye uongozi akitolea mfano wa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwanamke wa kwanza kuongoza Tanzania kama Rais.

Alisema Rais Samia ameonyesha njia, hivyo wanawake wengine hawanabudi kufuata nyao zake, na kwamba kwa sasa wanatakiwa kumuunga mkono ili aliongoze taifa kwa mafanikio.

"Mimi niko tayari kuwapa ushirikiano na kwa sasa naahidi kwamba kwa kutumia shule zangu za Paradise Mission Pre and Primary School na Patrick Mission, nitawasomesha bure masomo ya kidato cha tano na sita vijana 10 kutoka kwenye familia zenu ambao watafaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kupata daraja la kwanza," alisema Mwaselela.

Alisem anafanya hivyo ili kurudisha kwenye jamii kile anachopata kwenye uwekezaji wake katika elimu, akisema mapato anayopata ni kutokana na jamii, ambayo inapeleka wanafunzi.



## KCB yajipambanua na uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Benki ya KCB, Cosmas Mario, amesema benki hiyo inashirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kuhakikisha dhana ya uchumi wa bluu inatekelezwa kwa vitendo.

Aliyasema hayo juzi Mjini Zanzibar katika viwanja vya Amani, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mashindano ya mbio za "Zanzibar Blue Economy half Marathon 2021" ikiwa ni miongoni mwa maadhimisho ya sherehe za mwaka mmoja ya uongozi wa Rais Dk.Hussein Ali Mwinyi.

Alisema benki hiyo kwa miaka mitatu iliyopita imeshawezesha miradi yenye gharama za Sh. bilioni 60 na bado wanaendelea ambapo tayari kuna wawekezaji wa nje wanatarajia kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 500.

"KCB ni benki kubwa kuliko zote katika kanda ya Afrika Mashariki na ya kati na uzuri ya kwamba imeanzia hapa Zanzibar mwaka 1986 ikiwa inaitwa Bank of India," alisema.

Aliwataka wananchi kufika katika benki hiyo kupata huduma zinazotolewa na kushirikiana katika kujenga uchumi wa bluu ili kupata maendeleo.

Aidha, alisema benki hiyo inawaendeleza wajasiriamali kupitia kampeni ya tujiajiri ambayo inawaunga mkono vijana, kinamama na wajasiria mali wadogo kwa kuwapa elimu na mitaji ili kujiendeleza kimaisha na kiuchumi.

Akizungumza wakati akifungua mashindano hayo Rais Dk. Mwinyi alisema ili taifa liweze kufanikisha matarajio ya kukuza uchumi katika mwaka wa pili wa uongozi wake, halinabudi kuendelea kudumisha amani, uwajibikaji pamoja na watendaji kujenga uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akitoa maelezo kuhusu mashindano hayo, Mwenyekiti wa "Zanzibar Blue Economy half Marathon 2021", Abdalla Idrissa Majura, alieleza kwamba mashindano hayo ni kwa ajili ya kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kutimiza mwaka mmoja tokea aingie madarakani kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Majura alisema kuwa hatua hiyo imefikiwa baada ya kuonekana kwamba Rais Dk. Mwinyi ameanza kutekeleza ahadi zake kwa vitendo akiwa na lengo la kuiletea maendeleo Zanzibar.

# Dk. Mwinyi aainisha jitihada za kuufufua utalii dhidi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imefanya jitihada mbalimbali za kuifufua sekta ya utalii, baada ya kuathirika na janga la Uviko-19.

Akizungumzia mwaka mmoja wa mafanikio yake ya uongozi, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema hivi sasa kuna kampuni za ndege 34 zinazofanya safari Zanzibar zikiwamo kampuni mpya saba zilizoongezeka mwaka huu.

Alisema jitihada zilizochukuliwa kutafuta masoko mapya katika nchi za Ulaya Mashariki na Mashariki ya mbali zimesaidia sana ambapo Zanzibar imepokea watalii wengi kutoka Ukraine, Urusi na nchi zingine ambapo imewezesha hoteli nyingi kuwa wazi katika kipindi kigumu kwa sekta hiyo.

Alieleza kuwa jumla ya watalii 330,659 wameingia nchini kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi Agosti, 2021, ikilinganishwa na watalii 273, 852 walioingia Novemba, 2019 hadi Agosti, 2020, sawa na ongezeko la asilimia 17.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 95 ya hoteli zilizopo Zanzibar zenye nyota kuanzia moja hadi tano zilifungwa au kupunguza shughuli za uendeshaji kuanzia mwaka 2020 na kusababisha kupunguzwa wafanyakazi kwa zaidi ya asilimia 90.

"Kama tunavyojua kuwa maendeleo ya sekta ya utalii yamefungamana sana na maendeleo ya ukuaji wa sekta nyingine hapa kwetu. Kwa hivyo, kuanguka kwa utalii na kufungwa hoteli kuliathiri sekta ya kilimo, uvuvi, ufugaji, usafiri wa anga na nchi kavu, biashara na maendeleo ya makundi mbalimbali ya wajasiriamali," alisema na kuendelea:

"Hali hii imeleta mdororo wa uchumi wa nchi yetu na kupungua kwa kiasi kikubwa mzunguko wa fedha katika uchumi wetu."

Alisema katika maadhimisho hayo ya kutimiza mwaka mmoja amefungua na kuweka mawe ya msingi ya miradi mitatu mikubwa ya hoteli za kitalii za daraja la juu zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 3.15.

Aidha, alisema kwa lengo la kukuza uwekezaji katika sekta ya utalii imetangazwa fursa ya kuwekeza katika visiwa vidogo viliopo Zanzibar ambapo tayari maombi 54 ya wawekezaji wenye nia ya uwekezaji katika visiwa hivyo yamepokelewa.

"Fursa hiyo imetolewa kwa visiwa 10 ambavyo ni Njau, Pamunda 'A', Pamunda 'B', Bawe, Kwale, Changuu, Mtumbini, Chumbe, Misali na Chapwani," alisema.

Alieleza kuwa kwa upande wa Mji Mkongwe, serikali imechukua hatua mbalimbali za utunzaji na uendelezaji wa Mji Mkongwe, ili uendelee kuwa na hadhi ya urithi wa kimataifa.

Alisema serikali inaendeleza kazi ya kulifanyia matengenezo jengo la Beit al Ajaib baada ya kuanguka pamoja na Makumbusho ya Kasri la Wananchi Forodhoni na hivi sasa, kazi ya ujenzi wa kulizuwia jengo la Beit el Ajaib lisianguke inaendelea kwa kushirikiana na Serikali ya Oman ambayo imekubali kutoa Dola milioni 5.93 na kazi ya matengenezo makubwa ya jengo lote inatarajiwa kuanza Februari 2022.

Hata hivyo, alisema jitihada zimefanyika katika kuimarisha mapato yanayokusanywa na Shirika la Bandari ambapo kabla ya serikali yake kuingia madarakani, makusanyo kwa mwezi yalikuwa wastani wa Sh. bilioni 2.8 na faida ghafi ni wastani wa Sh. milioni 900.

" Hivi sasa, Shirika la Bandari linakusanya wastani wa Sh. bilioni 3.3 kwa mwezi na faida ghafi ya wastani wa Sh. bilioni 2, kiwango hicho kimepanda zaidi katika mwezi wa Oktoba, 2021 na kufikia makusanyo ya Sh. bilioni 4.2 na faida ghafi ya wastani wa Sh. bilioni 2.6," alisema Dk. Mwinyi.

Naye Mkurugenzi wa Bandari Zanzibar, Nahad Mahfoudh, alisema licha ya biashara kushuka duniani kutokana na janga la corona, lakini wamepita lengo la ukusanyaji wa mapato katika shirika hilo ambapo kwa Oktoba pekee wamekusanya Sh. bilioni 4.2, jambo ambalo miaka ya nyuma haijawahi kutokea.

Alisema jambo ambalo limefanikisha kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato ni ufanisi na uwajibikaji mzuri kwa watendaji na kuziba mianya ya rushwa katika shirika hilo.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema changamoto kubwa inayolikabili shirika hilo ni ufinyu wa Bandari ya Malindi, ambayo ilijengwa tokea mwaka 1920 wakati huo ikikidhi mahitaji ikilinganishwa na sasa.




Meneja wa Benki ya KBC tawi la Stone Town Zanzibar, Mbarouk Ramadan Mbarouk, akizungumza na waandishi wa habari ambao hawapo pichani baada ya mashindano ya riadha ya uchumi wa bluu yaliofanyika Amani Mjini Zanzibar, KCB ni miongoni mwa wadhamini wa mashindano hayo.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbunge apania kumaliza kikwazo cha maji Welezo

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Jimbo la Welezo Zanzibar, Maulid Saleh Ali, amesema amejipanga kumaliza tatizo la ukosefu wa majisafi na salama kwa baadhi ya maeneo ya jimbo hilo. Aliyasema hayo jana alipokuwa akishirikiana na wananchi na mafundi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kusambaza mabomba ya maji katika shehia za Mtopepo na Munduli kwenye jimbo hilo.

Alisema nishati maji ni muhimu kwa mahitaji ya kila siku ya wananchi na yanayatumia katika mambo mbalimbali ya msingi, hivyo ni lazima yapatikane muda wote bila usumbufu.

Alisema ataendelea kushirikiana na serikali kupitia mfuko wa jimbo kuhakikisha mahitaji yote ya msingi hasa majisafi na salama, elimu, huduma za afya, barabara za ndani na vikundi vya ujasiriamali kwa ajili ya kuwakwamua vijana na wanawake yote yanapatikana kwa wakati. Mbunge huyo aliwasisitiza wananchi hao kuwa walinzi wa miundombinu ya maji ili isihujumiwe na iweze kuendelea kuwanufaisha wananchi wengi na maeneo jirani.

"Jimbo letu lina sifa kubwa ya kuwa na vyanzo vingi vya maji ambayo siku za hivi karibuni wamekuwa wakinufaika wananchi wa maeneo mengine, huku baadhi ya maeneo ya jimbo letu yakikosa maji kutokana na changamoto za uchakavu wa miundombinu na uharibifu wa miundombinu hiyo na baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu," alisema.

Naye Diwani wa Wadi ya Munduli, Juma Fikirini Khamis, aliwasihi wananchi wa maeneo hayo yanayokabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji mradi huo mkubwa wa maji utakapokamilika wahakikishe wanajisajili na kufuata taratibu zilizowekwa na serikali. Alisema viongozi wa jimbo hilo hasa mbunge, mwakilishi na madiwani wanashirikiana vizuri kutatua changamoto za jimbo hilo kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Fundi kutoka ZAWA, Talib Abdallah Mohamed, alisema wanatarajia kutumia mwezi mmoja kukamilisha zoezi hilo na kuhakikisha wananchi hao wanapata huduma ya majisafi na salama.

# Wakimbizi wa Burundi, DRC wapata chanjo ya Uviko-19

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

MAMIA ya wakimbizi toka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC) wamejitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa Uviko-19 baada ya Serikali na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) kuanza kutoa huduma hiyo kwa mara ya kwanza kwa wakimbizi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Dk. Hosea William, alisema wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo kuwa zoezi hilo limeanza kwa kundi la wakimbizi baada ya taratibu zote kukamilika, ambapo chanjo inayotolewa ni aina ya Sinopharm, ambayo inatarajiwa kutolewa kwa zaidi ya asilimia 60 ya wakimbizi wenye umri wa kuanzia miaka 18.

Alisema kabla ya zoezi hilo wataalamu wa afya wa serikali na kutoka mashirika yanayotoa huduma kambini hapo, Chama cha Msalaba Mwekundu na Medical Team wamekuwa wakitoa elimu na uhamasishaji kwa wakimbizi.

Dk. William aliwataka wakimbizi kuendelea kujitokeza kupokea chanjo hiyo ili kujikinga na ugonjwa wa Uviko- 19 ambao ni janga la dunia kwa sasa.

Naye mkuu wa kambi ya wakimbizi Nyarugusu, Siasa Majenje, alisema kambi hiyo ina watu zaidi ya 128,000 ambao ni wakimbizi na waomba hifadhi toka nchi za Burundi na DRC na kwamba wameruhusu uhamasishaji ufanyike katika maeneo yote ya mikusanyiko ili kufikia malengo ya zoezi hilo.

Alisema tangu kuwapo kwa ugonjwa huo haijaripotiwa mkimbizi kuugua au kufa kutokana na Uviko-19, hivyo hatua ya kuwakinga kwa kuwapatia chanjo inawaweka katika mazingira sahihi ya kuepuka ugonjwa huo hatari.

Mkuu wa UNHCR Kasulu, Ben Diallo, alisema chanjo hiyo ni muhimu kwa wakimbizi katika kuhakikisha wanakuwa salama wakiwa ukimbizini.

Aliwataka kupuuza taarifa zisizo rasmi zinazosambazwa kuhusu chanjo hiyo kwa kuwa chanjo hiyo imehakikiwa na wataalamu na kuthibitishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na Serikali ya Tanzania.

Ameishukuru idara ya huduma kwa wakimbizi kuruhusu kutolewa chanjo kwa wakimbizi, ambapo alisema hatua hiyo inatoa haki kwa wakimbizi kuamua kuchanja kwa hiari.



Mkurugenzi wa Taasisi ya kiraia ya Community Hands Foundation (C-HF), Paul Makoe (kushoto), akitoa maelekezo kwa wanafunzi wakati wa uzinduzi wa mradi wa Elimika uliofanyika juzi, katika Shule ya Msingi Mchikichini iliyoko Mbagala mkoani Dar es Salaam. Kampeni hiyo itaendeshwa kwa miaka mitano ikiwa na lengo la kutoa elimu ya afya, maadili na malezi kwa wanafunzi na vijana ili kujiepusha na utovu wa nidhamu pia wanatarajia kufikia mikoa zaidi ya 20 nchini. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Tani 2,000,782 korosho zauzwa kwa mfumo stakabadhi ghalani

**Na Yasmine Protace,** IKWIRIRI

MKOA wa Pwani, umefanikiwa kuuza tani milioni mbili za korosho kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Hayo yalisemwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mkoa (CORRECU), Dullar Chaulembo, alipokuwa akizungumza na wawakilishi wa vyama vya msingi vya Ushirika (AMCOS) Mkoa wa Pwani katika mnada wa tatu uliofanyika Ikwiriri, Wilaya ya Rufiji.

Alisema wakulima wa korosho Mkoa wa Pwani, wanaipongeza serikali, kufuatia mikakati yake ambayo imechangia korosho zao za daraja la kwanza msimu huu kufikia kwa asilimia 85.

"Tunaipongeza serikali kupitia mikakati yake, ambayo imesaidia kupatikana kwa korosho zenye ubora wa juu daraja la kwanza kufikia asilimia 85," alisema.

Pia aliwashukuru wakulima wa korosho kuzingatia maelezo ya Bodi ya Korosh (CBT) yanayolenga kuboresha korosho zao, huku akiwataka wakulima kuongeza juhudi zaidi katika uzalishaji wa zao hilo.

Akitangaza bei za mnada huo, ambao wakulima walilidhia, Meneja wa CORRECU, Hamis Mantewela, alisema bei ya korosho daraja la kwanza ilikuwa Sh. 2,55.11, huku daraja la pili likiuzwa kwa Sh. 1,700.99.

"Kutokana na kuwapo kwa bei mbili kati ya korosho daraja la kwanza na korosho daraja la pili, tumefanikiwa kuuza tani 2,000,782," alisema.

Mkulima wa zao hilo kutoka Mkuranga, Said Njomoke, alisema wanaiomba serikali iendelee kuwahamasisha wanunuzi wanunue zao hilo ikiwamo kuwaongezea bei.

# Wanaofanya kazi ofisini hatarini kuugua magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu,** Arusha

WANAOFANYA kazi ofisini wako katika hatari ya kuugua magonjwa yasiyoambukiza.

Hayo yamesemwa juzi na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, alipokuwa akifungua wiki ya magonjwa yasiyoambukiza, inayoadhimishwa kitaifa mkoani hapa.

"Wafanyakazi wa serikali wapo hatarini kuugua magonjwa yasiyoambukiza kutokana na kutumia muda mrefu kufanya kazi ofisini," alionya na kuongeza pia kuwa wakati wa kwenda na kutoka ofisini hutumia magari.

Alisema kuwa wataalamu wa afya wanaonya kuwa watu wasiofanya mazoezi mara kwa mara wanakuwa hatarini kuugua magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema kwamba wafanyakazi wengi wa ofisini huwa wametingwa na mambo mengi wanayopaswa kuyakalimisha kila siku na kufanya kazi wakiwa wamekaa kwa muda mrefu na hawana muda wa kushughulisha miili yao.

Alisema kama mtu hafanyi mazoezi na anakula mara tatu kwa siku, chakula hicho huwa hakitumiki kikamilifu na badala yake kujirundika mwilini na kuwa chanzo cha magonjwa.

Alisema mazoezi hufanya mwili kutumia chakula cha ziada mwilini na kuufanya mwili kuwa mkakamavu.

Kwa sababu hiyo alihamasisha Watanzania kujitengea utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara.

Katika hatua nyingine aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali kuhakikisha kwenye maeneo yao kuna maeneo na viwanja vya wazi ili kufanya mazoezi na kuhakikisha matembezi ya mchakamchaka na michezo inahimizwa shuleni.

Alisema kaulimbiu ya Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza mwaka huu ni 'Badili Mtindo wa Maisha Boresha Afya' ukilenga kuhamasisha jamii kuacha mitindo na tabia zinazochochea magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema mbali na kuzingatia kufanya mazoezi, ni vyema kula mlo kamili na kupunguza kwenye vyakula wingi wa mafuta, sukari na chumvi.

Alisema kuwa takwimu za magonjwa yasiyoambukiza zinaonyesha kuwa yanachangia vifo vya watu milioni 41 kila mwaka ulimwenguni sawa na asilimia 75 ya vifo.

HABARI KIMATAIFA

## Waziri Mkuu Iraq anusurika kifo jaribio la mauaji nyumbani kwake

**Baghdad,** IRAQ

WAZIRI Mkuu wa Iraq, Mustafa al-Khadhimi, amenusurika jaribio la mauaji lililofanywa kwa kutumia ndege zisizo rubani, zenye silaha zilizoyalenga makazi yake katika Ukanda wa Kijani wenye ulinzi mkali mjini Baghdad.

Maofisa wa serikali yake wanasema, Khadhimi hakudhurika kutokana na mashambulizi hayo yaliyofanyika mapema, jana.

Mashambulizi hayo ni ishara ya hali kuelekea kubaya zaidi iliyochochewa na wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran, kukataa kuyatambua matokeo ya uchaguzi wa ubunge wa mwezi uliopita.

Maofisa wawili wa serikali ya Iraq, waliliambia shirika la habari la AP kwamba, walinzi saba wa Khadhimi walijeruhiwa kwa mashambulizi ya ndege mbili zenye silaha zisizo rubani, yaliyotokea kwenye eneo mashuhuri la Ukanda wa Kijani, ambalo kawaida linakuwa na ulinzi mkali.

"Maroketi ya wahaini hayatatuondosha hata hatua moja kwenye msimamo wetu na dhamira ya walinzi wetu mashujaa."

Khadhimi aliandika kwenye ukurasa wa Twitter muda mfupi baada ya mashambuli hayo.

"Niko salama na nipo baina ya watu. Alhamdulillah!"Vyuo vikuu vyote 282, vyuo vya ufundi na taasisi nyingine za elimu ya juu kote nchini vinakabiliwa na changamoto zinazofanana. **BBC**

ONGEZEKO LA JOTO, UKAME:

# Dunia kubuni nyama, protini mbadala kutoka maabara

**Glasgow,** SCOTLAND

DUNIA ikiwa katika mjadala mkubwa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, kwenye mkutano wa kilele wa hali ya hewa wa COP26, unaojumuisha viongozi wa mataifa makubwa duniani, wataalamu wa teknolojia ya chakula wanatafuta jawabu la protini mbadala na namna ya kutumia katika vita dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Watafiti katika nchi nyingi wanatafuta mbadala wa nyama (kama chanzo kikuu cha jadi cha protini kwa sasa), kwa kuwa mifugo ni moja ya sababu za ongezeko la joto duniani.Wazo la protini mbadala linaungwa mkono hata na nyota wa filamu za Hollywood, Leonardo DiCaprio.

Desemba 2020, Singapore ilikuwa nchi ya kwanza duniani kuanza kuuza nyama inayozalishwa katika maabara.

Teknolojia hiyo ni kwamba, wanasayansi huchukua seli kutoka kwa misuli ya mnyama au tishu za 'adipose' na kuzipandikiza maabara katika mazingira rafiki ya ukuaji.

Kampuni ya 'Eat Just now' yenye makao yake huko San Francisco, Marekani, inauza nchini Singapore kuku waliozalishwa kwenye maabara.

Hii ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa usalama wa nchi, unaolenga kupunguza utegemezi wa kuagiza chakula kutoka kwa majirani zake.

Wachambuzi wanatarajia kuwa katika miaka michache ijayo, wazalishaji wa nyama bandia ya Uholanzi, Moas Meat and Meatable, watajaribu kupata kibali kutoka kwa wasimamizi wa Umoja wa Ulaya, ili kuzalisha kwa wingi na kuuza Ulaya, nyama hiyo ya maabara.

Hatua kubwa zaidi zinatarajiwa kuchukuliwa na wazalishaji wa Marekani, Memphis na New Age Meats, ambayo ina mkono wake kwenye taasisi ya Bill Gates. **BBC**



Familia ikisafiri na kuyaacha makazi yao kutokana na mafuriko baada ya mvua kubwa eneo la Bandung, nchini Indonesia, juzi. Nchi za bara la Asia zimeendelea kushuhudia mvua kubwa zikinyesha na kuathiri maeneo kadhaa kutokana na mabadiliko ya tabianchi duniani. **PICHA: REUTERS**

# Rais Paul Biya ajivunia miaka 39 madarakani

**Yaounde,** CAMEROON

WAFUASI wa kiongozi wa pili kwa kuwepo madarakani kwa muda mrefu barani Afrika, Rais Paul Biya wa Cameroon mwenye umri wa miaka 88 wamesherehekea kuwapo kwake katika uongozi kwa miaka 39.

Biya, ambaye amekuwa rais wa Cameroon tangu mwaka 1982, ni nadra sana kuonekana hadharani.

Wafuasi wa chama tawala cha Cameroon, Cameroon Peoples' Democratic Movement (CPDM), wamekuwa wakisherehekea mwishoni mwa wiki, uongozi wa Rais Biya na kusema, anaweza bado kutawala taifa hilo la Afrika ya Kati kwa miaka mingine saba kuanzia mwaka 2025.

Biya alitangazwa mshindi katika uchaguzi wa mwaka 2018 akiwa amepata zaidi asilimia 80 ya kura.

Mijini na vijijini kote Cameroon, watu walikuwa wakiimba kusherehekea uongozi wa miaka 39 wa Biya.


Tukio moja lilifanyika Monatele, mji mkuu wa Lekie, idara iliyo karibu na mji mkuu wa Cameroon, Yaounde.

Henri Eyebe Ayissi, Waziri wa Mali za Taifa, Utafiti na Milki ya Ardhi na mshirika wa karibu wa Biya, aliongoza ujumbe wa chama cha CPDM, kwenda Lekie na kuwasilisha kile alichokiita ni ujumbe maalum wa mfuasi wa Biya.

Ayissi alisema CPDM inaomba yawepo maridhiano ya kitaifa kwa Biya kuwania awamu mpya ya uongozi mwaka 2025.

Alisema wanamwomba Biya akubali wito wa kuwania tena urais mwaka 2024 na kuendeleza kazi nzuri anayoifanya Cameroon.

"Biya ameendeleza umoja licha ya ugaidi wa Boko Haram kwenye upande wa kaskazini mwa Cameroon kwenye mpaka na Nigeria na mzozo wa wale wanaotaka kujitenga ambao umesababisha vifo vya takriban watu 3,000 katika mikoa inayotumia lugha ya Kiingereza," alisema Ayissi.



Ayissi alisema mamilioni ya watoto nchini Cameroon wana fursa ya elimu kwa sababu, Biya amejenga shule na vyuo vikuu katika miji na vijiji kadhaa katika taifa hilo la Afrika ya Kati.

Wito wa Biya kuwania tena urais wakati muhula wake wa sasa wa miaka saba unamalizika mwaka 2025, umeungwa mkono katika miji kadhaa na vijiji mbali mbali, na kuchochea ukosoaji mkubwa kutoka kwa wapinzani wa Biya.

Christopher Ndong ni Katibu Mkuu wa Cameroon Renaissance Movement, chama ambacho kinadai kuwa mgombea wake, Maurice Kamto, alishinda uchaguzi wa mwaka 2018 na kwamba, Biya aliiba ushindi wake.

Ndong alidai, kumtaka Biya kuwania tena uongozi mwaka 2025 kuna maana kuwa, CPDM inataka kiongozi huyo afie madarakani.

"Ni kudharau Wacameroon na demokrasia ya nchi hii. Kutokana na umri wake, atafanya nini akipewa tena madaraka? Hivi sasa, hajishughulishi.

Kwa kweli, huu ni uchochezi kwa utaratibu. Angalia vurugu zote ambazo zinatokea. Nchi ina madeni. Kwa kweli, inaonyesha kwamba hakuna mtu katika uongozi. Wito wa mwaka 2025 usitiliwe maanani kwasababu tunafahamu kuwa hali na afya ya mkuu wa nchi haitamruhusu kutawala nchi hii mwaka 2025."

Ngole Ngole Elvis, Mkuu wa Chuo cha Chama cha CPDM na mshauri wa karibu wa Biya, anasema wito kwa Biya kuwania tena ni wa kidemokrasia.

Alisema badala ya kulalamika kwamba Biya amekuwapo madarakani kwa muda mrefu, upinzani ni vyema ujitayarishe kwa upigaji kura wa kidemokrasia badala ya kusema wanadhani nani anafaa kuwania urais mwaka 2025.

Biya alihudumu kama waziri mkuu kwa miaka saba, kabla ya kuwa rais. Mwaka 2008, aliondoa katika katiba viwango vya rais kuhudumu na kumruhusu kuwania kwa kipindi kisichokuwa na kikomo.

Hivi sasa ni kiongozi wa pili kwa kuhudumu kwa muda mrefu madarakani barani Afrika chini ya Jangwa la Sahara, wa kwanza ni jirani yake, Rais wa Equatorial Guinea Theodoro Obiang Nguema ambaye ameshikilia madaraka, tangu mwaka 1979. **VOA**

HABARI MICHEZO

# MASHABIKI SOKA WAKUNWA 'NJE YA DIMBA NA STARS'

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka na timu ya Taifa, Taifa Stars, wameeleza kufurahishwa na Kampeni ya 'Nje ya Dimba na Stars' inayoendeshwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), kupitia bia yake ya Serengeti Lager.

**Kampeni hiyo iliyozinduliwa hivi karibuni ambayo itadumu kwa kipindi cha miezi mitatu, inalenga kuwapa nafasi mashabiki wa Taifa Stars kukutana na nyota wanaowapenda katika baa zao na pia kutoa fursa kwao ya kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya soka pamoja na kupiga nao picha za ukumbusho.**

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, baadhi ya mashabiki wamesema kampeni hiyo imeweza kukata kiu yao ya kuwaona na kuongea na wachezaji nyota ambao huishia kuwaona uwanjani au kwenye vyombo vya habari.

Mohammed Salum maarufu kama 'Mudi', ambaye ni mmoja kati ya mashabiki waliojitokeza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam, amesema hakuamini kama ipo siku anaweza kukutana na wachezaji nyota wenye majina makubwa uso kwa uso na kuongea nao na kisha kupiga nao picha.

"Nilishangaa, lakini nilifurahi kukutana na wachezaji wakubwa kama Feisal Salum, Kibu Denis, Erasto Nyoni na wengine. Kwa hali ya kawaida siyo rahisi sana kukutana nao nje ya uwanja na kupiga nao picha,"alisema.

Shabiki mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Agness Manka, alisema bia ya Serengeti imefanya jambo ambalo litawafanya mashabiki kuzidisha mapenzi kwa timu yao ya taifa kupitia kuwaona wachezaji wanaowapenda.

"Mimi mara nyingi nimekuwa nikiwaona wachezaji nyota wa Taifa Stars kwenye vyombo vya habari kama TV na magazeti. Sikuwahi kuwaza kama naweza kukutana nao uso kwa uso na hata kupiga nao picha,"alisema.

Meneja mwandamizi wa chapa ya SBL, Wankyo Marando, amesema Bia ya Serengeti Lager ikiwa kama shabiki mkuu wa Taifa Stars, inajivunia kuwaletea mashabiki wa Taifa Stars nyota wanaowapenda na kuwapa nafasi ya kuzungumza nao na hivyo kuwafahamu kwa undani zaidi.

Wankyo alisema kampeni hiyo ya nchi nzima itahusisha wachezaji wa Taifa Stars ambapo watatembelea mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha na kukutana na mashabiki wao kupitia matukio kama pati za mwisho wa mwezi 'Nje ya Dimba na Stars'. Kwenye matukio kama hayo mashabiki wataweza pia kujishindia zawadi mbalimbali na ofa za bei yao pendwa ya Serengeti Lager.

"Wachezaji watakuwa kwenye baa mbalimbali na wakati wateja wetu wa bia ya Serengeti Lager wakiendelea kuburudika na bia yao pendwa iliyotengenezwa kwa kimea kwa asilimia 100 na isiyoongezwa sukari, watapata nafasi ya kuwauliza maswali, kupiga picha na kupata sahihi zao," alisema.



Baadhi ya mashabiki wa Timu ya Taifa ya Tanzania, wakiwa pamoja na baadhi ya wachezaji nyota wa timu hiyo baada ya uzinduzi wa Kampeni ya 'Nje ya Dimba na Stars' uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Coastal kusajili straika Mzambia

**Na Adam Fungamwango**

ILI kukifanyia marekebisho kikosi chao, klabu ya Coastal Union iko hatua ya mwisho ya kumalizana na straika raia wa Zambia anayecheza soka la kulipwa Afrika Kusini, atakayejiunga na timu hiyo kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili wa klabu hiyo, Ahmed Aurora, amesema wameamua kuingia sokoni kutafuta straika baada ya kuona ndiyo nafasi inayowasumbua kwa sasa kwenye kikosi chao.

Alisema kwa sasa hawezi kulitaja jina la mchezaji huyo, lakini mchakato umefikia asilimia 80 na ukishakamilika watamtangaza rasmi. Kuhusu usajili msimu huu, alisema wapo wachezaji ambao ni wazuri, lakini baadhi yao hawana hadhi hiyo na walidanganywa kwenye majaribio.

## Netiboli na matumaini kibao michuano Afrika

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Netiboli, imeondoka leo alfajiri kuelekea nchini Namibia, ikiwa na matumaini kibao ya kufanya vizuri katika mashindano yanayoshirikisha nchi za Afrika yanayotarajiwa kuanza kesho hadi Novemba 16, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli nchini (CHANETA), Devota Marwa, alisema baada ya uongozi wao kuingia madarakani, wamehakikisha wanalipa ada iliyokuwa inadaiwa ili kwenda kushiriki michuano hiyo.

Alisema wamepata nafasi hiyo na timu inayoundwa na wachezaji 12 kutoka Tanzania Bara na Visiwani inaondoka kwenda kuiwakilisha vema nchini kwa kuhakikisha wanarejea na ushindi katika mashindano hayo ambayo hawakushiriki kwa miaka sita.

# *Washindi Shindano la ma-DJ hawa hapa*

**Na Mwandishi Wetu,** Arusha

HATIMAYE bia pendwa ya Serengeti Lite, imehitimisha shindano lake la 'DJs' lililopewa jina la 'Take a Bite Out of Life' kwa kuwatunuku ma-DJ watatu bora nchini vifaa vya kupigia muziki vyenye thamani ya Sh. milioni saba kila mmoja, tukio hilo likifanyika Ukumbi wa Triple-A kwa kushindanisha washiriki saba wa mwisho kutoka kanda tofauti nchini.

Tukio hilo lilihitimisha kampeni ya miezi mitatu kwa kupata ma-DJ watatu kutoka kanda saba nchini. Pia washindi hao wamepata fursa adimu za kuwa ma-DJ rasmi wa chapa ya Serengeti Lite katika promosheni na shughuli zake za utangazaji nchini.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha hafla hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Bia cha SBL, Nandy Mwiyombella, kwanza aliwapongeza washindi hao; Abduliazizi Juma 'Dully TZ' kutoka Dodoma, aliyeshika nafasi ya kwanza, Steven Jonathan 'DJ Stegio wa Dar es Salaam na Mussa Shaban 'DJ Son' kutoka Kilimanjaro.

Alisema: "'Ni wakati wa kusisimua kwa SBL na bia yake ya kipekee, Serengeti Lite, ambayo imetumia shindano hili ili kuwasaidia vijana kuonyesha vipaji vyao. Serengeti Lite ina shauku ya kuwaona vijana wakionyesha umahiri wao katika vipaji walivyonavyo.

"Vilevile shabaha ya 'Take a Bite Out of Life', ililenga kutoa burudani kwa wateja wetu katika maeneo waliyopo ili waendelee kufurahia kinywaji chenye ladha kamili cha Serengeti Lite, Bia ya Kitanzania iliyotengenezwa kwa ajili ya Watanzania na ya Watanzania."

Ofisa Vijana wa Arusha, Japhet Kurwa, ndiye aliyeongoza hafla hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, John Mongella, ambaye pia aliwatunuku washindi watatu waliobahatika huku akipongeza juhudi za SBL za kuchochea soko la ajira kwa kutoa motisha kwa vijana kupitia sekta ya burudani.

"Nimejawa na furaha kubwa sana baada ya kushuhudia jinsi vijana wanavyopambania ndoto zao kwa nguvu na ari. Nawapongeza sana SBL kwa kutimiza ndoto zao, ni siku nzuri kwa washindi hawa watatu; maisha yao hayatakuwa sawa tena kwa sababu fursa hii imekuwa chanzo cha ajira kwao. Nina uhakika pia kuwa washiriki wengine (hasa washindi) mtaanza kupokea mialiko mingi kwenye hafla za kutumbuiza muziki maeneo mbalimbali na pengine kufungua studio zenu za muziki hapo baadaye.

Kampeni ya Take a Bite Out of Life iliambatana na shughuli za burudani kutoka kwa ma-DJs wa ndani walioshindana katika wilaya na mikoa nchini kote ambapo shindano hilo lilishirikisha zaidi ya washindani 5,200 wenye zaidi ya miaka 18 na matarajio ya kujenga vipaji vyao kama wabudishaji wa muziki.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VINICIUS JR KUFUNGWA

REAL Madrid itaweka kipengele cha kumruhusu Vinicius Jr, 21, cha euro bilioni moja itakapompa mkataba mpya mshambuliaji huyo Mbrazil mwishoni mwa msimu. ***(AS)***

### NEWCASTLE YASUASUA

HATUA ya Newcastle United kumtangaza Eddie Howe kama kocha wao mpya inasuasua baada ya kushindwa kuafikiana na Jason Tindall ili awe msaidizi wa Howe. ***(90 Min)***

### RANGNICK KUMRITHI OLE

MANCHESTER United imemweka kocha wa zamani wa RB Leipzig, Ralf Rangnick katika orodha yake ya watakaorithi mikoba ya Ole Gunner Solskjaer iwapo atatimuliwa na Mjerumani huyo anavutiwa na mpango wa kuchukua kazi hiyo Old Trafford. ***(Christian Falk, Bild Sport head of football)***

### CONTE KUIBOMOA INTER

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte amekuwa akihusishwa kutaka kusajili wachezaji kutoka klabu yake ya zamani ya Inter Milan. ***(Football Italia)***

### MERINO ANYATIWA LIVER

KIUNGO wa Real Sociedad na Hispania, Mikel Merino, 25, ananyatiwa na Liverpool ili kuboresha kikosi chao huku dau la usajili la nyota wa kimataifa wa England anayechezea Borussia Dortmund, Jude Bellingham, 18, likionekana kuwa kubwa kwa 'Wekundu' hao wa Anfield. ***(Fichajes.net)***

### EVERTON HAITASAJILI

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amepuuzia kwamba klabu hiyo ya Goodison Park itamwaga fedha ya usajili katika dirisha la Januari. ***(Times)***

### SHEVCHENKO ATAJWA GENOA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea, Andriy Shevchenko anatarajiwa kutangazwa kuwa kocha mpya wa Genoa baada ya klabu hiyo kumtimua Davide Ballardini. ***(La Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

### KUINOA MIDDLESBROUGH

KOCHA wa zamani wa Sheffield United, Chris Wilder amekubali kuchukua mikoba ya kuinoa Middlesbrough baada ya kuondoka kwa Neil Warnock klabuni hapo. ***(Teesside Live)***

### JUVE WAMTAKA WITSEL

JUVENTUS huenda ikatupa ndoano zake kwa kiungo wa Borussia Dortmund na Ubelgiji, Alex Witsel, 32, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Bild, via 90 Min)***

### INSIGNE KUAMUA

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, 30, amesema uamuzi uko kwa mshambuliaji wa Italia, Lorenzo Insigne kama ataamua kusalia kwenye klabu hiyo ya Serie A ama la, huku mkataba wa nyota huyo ukielekea ukingoni mwishoni mwa msimu ujao. ***(Calciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER: MAN UNITED ITARUDI KWENYE UBORA

**Kiwango kilichoonyeshwa leo (juzi) hakikuwa cha kuvutia kabisa, lakini naamini...**

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anaamini kwamba, anaweza kuirudisha Manchester United kwenye kiwango chake licha ya kuchezea kichapo kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City, juzi Jumamosi.

**'Mashetani Wekundu' hao walipigwa 2-0 pale kwenye dimba la Old Trafford kwa mabao ya, Bernardo Silva na lile la kujifunga la Eric Bailly.**

Kichapo hicho kilikuwa cha sita kwa United katika mechi 12 zilizopita kwenye mashindano yote na cha nane nyumbani kwa mwaka 2021, ikiwa ni mara ya kwanza tangu mwaka 1989.

Wameruhusu nyavu zao kutikiswa katika mechi 14 mfululizo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1950, huku wakiruhusu mabao 11 katika mechi za nyumbani kwa msimu wa 2021-22.

Alipoulizwa kuhusu mambo yanavyoendelea ndani ya kikosi cha Man United, Solskjaer alisema: "Ukweli mambo hayako sawa. Tunahitaji kubadilisha matokeo na kuwa kwenye kiwango chetu.

"Kwa upande wangu naamini tutarudi kwenye kiwango chetu na mambo yatakuwa sawa kabisa.

"Kuna wakati kwenye soka mambo huwa yanakuwa magumu, lakini naamini kwamba tutarudi katika ubora wetu. Hii ni timu kubwa na itakuwa katika nafasi yake.

"Tumekuwa na wiki mbili au tatu ambazo hazifurahishi. Kiwango kilichoonyeshwa leo (juzi) hakikuwa cha kuvutia kabisa, lakini naamini mambo yatabadilika tu."

MECHI KALI
HOME AWAY
TENERIFE
2.13 | 3.14 | 3.43
GIRONA
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (watatu kushoto), akikabidhi zawadi ya fedha taslimu kwa mshindi wa mbio za NBC Dodoma Marathon Km. 21, Alphonce Simbu (wapili kushoto) zilizofanyika jana jijini Dodoma. Wanaoshuhudia ni Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (watatu kulia), Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo (wapili kulia) na Rais wa Shirikisho la Riadha Taifa (RT), Silas Isangi (kulia). **NA MPIGAPICHA WETU**

# NBC Marathon zakusanya mil. 200/- mapambano ya saratani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MBIO za hisani za kimataifa zilizoandaliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) "NBC Dodoma Marathon", zimefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa kinamama huku ikishuhudiwa wanariadha kutoka Tanzania wakifanya vizuri zaidi kwenye mashindano hayo kwa kuibuka vinara kwenye mbio za Km. 42 na Km. 21.

Katika mbio hizo zilizofanyika jijini Dodoma jana na kupambwa na uwapo wa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ilishuhudiwa Mwanariadha Mtanzania Tumaini Habie, akiibuka mshindi wa kwanza kwenye mbio za Km. 42 upande wa wanaume baada ya kumaliza kwa muda wa saa 02:17:15, akifuatiwa na mshiriki kutoka nchini Kenya, Eyanae Paul aliyetumia muda wa saa 02:18:31.

Mtanzania Abrahamu Too alimaliza katika nafasi ya tatu kwa kutumia muda wa saa 02:19:04

Upande wa wanawake mshindi wa kwanza katika mbio za Km. 42 ni Mkenya Cheruto Isgah, aliyetumia muda wa saa 02:45:03 akifuatiwa na Watanzania Jackline Sakilu na Sara Ramadhani waliotumia muda wa saa 02:45:46 na 02:46:13 kila mmoja.

Mwariadha wa Kimataifa kutoka Tanzania, Alphonce Simbu, aliibuka mshindi wa kwanza kwenye mbio za Km. 21 baada ya kumaliza kwa muda wa saa 01:03:46, akifuatiwa na Watanzania wengine katika nafasi ya pili na ya tatu ambao ni Joseph Panga pamoja na Daniel Giniki waliotumia muda wa saa 01:04:18 na 01:05:37 kila mmoja.

Upande wa wanawake, mshindi wa kwanza katika mbio za Km. 21 ni Mtanzania Failuna Abdi aliyetumia muda wa saa 01:14:50 akifuatiwa na Wakenya Lelei Jepkemboi na Tanui Euliter waliotumia muda wa saa 01:15:18 na 01:17:21

Katika mbio hizo ilishuhudiwa mshindi wa kwanza wa kilometa 42 kwa wanaume na wanawake kila mmoja akiondoka na Sh. milioni 5.5 huku upande wa kilometa 21, mshindi akiondoka na kitita cha Sh. milioni 3.5, wakati katika kilometa 10, mshindi akibeba Sh. milioni 1.5 na mshindi wa kilometa tano akizawadiwa Sh. milioni moja.

Akikabidhi hundi ya mchango huo yenye thamani ya Sh. milioni 200 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage, pamoja na zawadi kwa washindi wa mbio hizo, Waziri Bashungwa pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa kuandaa vema mbio hizo, alisema licha ya faida nyingine za kimichezo umuhimu wa mbio hizo unapimwa zaidi katika lengo lake la kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa kinamama.

"Tangu kuanzishwa kwa mbio hizi huu ukiwa ni msimu wa pili sasa, serikali imekuwa mstari wa mbele kuziunga mkono kutokana na dhima yake kuu ya kuwasaidia kina mama dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Tunashukuru kuona nia hiyo imefanikiwa na sasa tunakwenda kuokoa maisha ya maelfu ya kina mama kupitia jitihada za kimichezo." alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, aliwashukuru washiriki pamoja na wadhamini wa mbio hizo kwa kufanikisha lengo kuu la kuchangia huduma za afya katika Hospitali ya Ocean Road, hasusan matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi, ambayo ndiyo inayoongoza kwa vifo vitokanavyo na saratani nchini.

"Ndio maana pamoja na yote tunatumia fursa hii kujipongeza sisi sote tukiwamo waandaaji, washiriki pamoja na wadhamini wetu kwa kufanikisha lengo hili muhimu. Pamoja na kwamba tumepata washindi wa mbio hizi, lakini bado kila mshiriki ni mshindi kwa sababu amefanikisha kuokoa maisha ya mama zetu," alisema.

Akipokea msaada huo Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage aliishukuru benki hiyo kwa jitihada hizo huku akibaisha kuwa msaada huo unakwenda kusaidia mapambano hayo katika maeneo mbalimbali hususan mikoani ili kuwahi matibabu kwa wagonjwa ambao wamekuwa wakifika hospitalini wakiwa katika hatua ya mwisho ya ugonjwa huo.





# MBAPPE: PSG BADO HAIJAWA BORA KWA SASA

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema Paris Saint-Germain bado inahangaika kurudi kwenye kiwango chake msimu huu, lakini amesisitiza hakuna haja ya kupaniki.

Kikosi hicho cha kocha Mauricio Pochettino kinaongoza msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa kwa pointi 10 kwenye msimamo wa Ligue 1 baada ya kupata ushindi mgumu wa mabao 3-2 ugenini dhidi ya Bordeaux, Jumamosi.

Walionekana kama wangeondoka na ushindi wa rahisi wakati wakiongoza kwa 3-0, huku Neymar akifunga mara mbili kipindi cha kwanza, mabao yote yakitengenezwa na Mbappe.

Mbappe akafunga la tatu na kufanya matokeo kuwa 3-0 kipindi cha pili, lakini yakarudi mawili yaliyofungwa na Alberth Elis na M'Baye Niang.

Na Mbappe baada ya mchezo huo alisema kwamba, PSG bado haijawa kwenye kiwango chake bora msimu huu, lakini hakuna haja ya kupaniki kwa sababu msimu bado ni mrefu.

"Hatukuwa bora, mchezo haukuwa mgumu sana, lakini sisi wenyewe ndio tuliufanya hivyo," alisema Mbappe akiiambia Canal+.






...shindi wa bonus ya Jackpot, Raymond Chaula, ...toka Lindi akionyesha mfano wa hundi ...Sh. milioni tano, baada ya kubashiri kwa ...ahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya ...ortPesa wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# *Ancelotti anaamini Xavi ataipaishia Barca*

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anatarajia Barcelona kurudi kwenye kiwango chake baada ya kuwa na mwanzo mbaya msimu huu chini ya kocha mpya, Xavi.

Xavi leo Jumatatu anatarajiwa kutangazwa kuwa kocha mpya wa miamba hao wa LaLiga kuchukua mikoba ya Ronald Koeman aliyetimuliwa hapo Camp Nou.

Barca wamepitwa pointi 10 na Madrid baada ya Jumamosi kulazimishwa sare ya mabao 3-3 na Celta Vigo, huku vijana hao wa Ancelotti wakiongoza ligi baada ya kushinda 2-1 dhidi ya Rayo Vallecano siku hiyo hiyo.

Ancelotti aliulizwa kuhusu kurudi kwa gwiji wa Barca, Xavi hapo Katalunya - huku timu hiyo ikiwa nafasi ya tisa kwenye msimamo na alisema:

"Kikawaida sitaki kuzungumza kuhusu Barcelona, najua kwamba wapo kwenye wakati mgumu kwa sasa na nimesema hivyo mara kadhaa kwa sababu ni klabu ninayoiheshimu, na ninatarajia Xavi atafanya vizuri," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Namtakia kila la heri kwa sababu naamini kwamba huu ni wakati wa mpito tu kwao, lakini bado wana ubora wa kutosha kuweza kuwa kwenye kiwango chao."

Ancelotti aliongeza: "Ni jambo la kushangaza kwamba tunaongoza kwa tofauti ya pointi 10 dhidi ya Barcelona, lakini nafikiri Barcelona wanaweza kurudi kwenye ubora wao haraka zaidi."


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 08 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1711 | Alashkert Martuni vs Urartu | 2.11 | 3.08 | 3.32 |
| 14:30 | 4762 | Al Sareeh vs Manshia Bani Hassan | 1.04 | 9.63 | 28.89 |
| 15:00 | 2814 | FK Radnicki 1923 vs Mladost Lucani | 2.18 | 3.38 | 2.90 |
| 15:15 | 5028 | FC Podillya Khmelnytskyi vs Volyn Lutsk | 2.59 | 2.93 | 2.69 |
| 15:30 | 5589 | Ludogorets Razgrad B vs Hebar Pazardzhik | 3.19 | 3.24 | 2.10 |
| 15:45 | 2246 | CA Fenix vs IA Sud America | 1.92 | 3.48 | 3.43 |
| 15:45 | 4922 | Egnatia Rrogozhine vs Vllaznia | 2.56 | 2.95 | 2.70 |
| 16:00 | 2148 | Barnsley U23 vs Hull City U23 | 2.09 | 3.71 | 2.84 |
| 17:30 | 5260 | AL Sahel SC vs AL Ain | 2.70 | 3.10 | 2.70 |
| 17:35 | 3794 | AL Jeel vs Ohud Medina | 2.60 | 3.10 | 2.85 |
| 18:30 | 2344 | CSKA Sofia vs CSKA 1948 | 1.40 | 4.33 | 6.55 |
| 18:30 | 4313 | Universitatea Cluj vs FC Brasov Steagul Renaste | 1.34 | 4.64 | 7.15 |
| 19:30 | 2112 | Alliance Lypova Dolyna vs FC Obolon Kiev | 2.20 | 3.18 | 3.03 |
| 19:40 | 4929 | Al Wehda vs Al Qadisiyah | 2.22 | 3.08 | 3.08 |
| 20:00 | 2326 | Sloboda Tuzla vs Velez Mostar | 2.22 | 3.04 | 3.13 |
| 20:00 | 3196 | Hapoel Ramat Gan vs Hapoel Acre | 2.31 | 3.02 | 3.27 |
| 20:00 | 4410 | Bnei Yehuda vs Sectzya Nes Ziona | 1.72 | 3.52 | 4.86 |
| 20:00 | 4771 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Raanana | 1.69 | 3.55 | 5.40 |
| 21:00 | 2184 | FC Helsingor vs FC Fredericia | 1.87 | 3.66 | 3.42 |
| 21:00 | 2604 | Kickers Wurzburg vs Eintracht Braunschweig | 3.08 | 3.23 | 2.24 |
| 21:00 | 3489 | Nacional Madeira vs GD Chaves | 2.26 | 3.26 | 2.97 |
| 21:30 | 1099 | FV Dudenhofen vs FC Speyer 09 | 1.15 | 7.12 | 11.55 |
| 21:30 | 4488 | Clinceni vs Rapid Bucuresti | 3.63 | 3.14 | 2.06 |
| 21:30 | 5350 | Oostende U21 vs Jeugd Rfc Seraing United U21 | 1.52 | 4.43 | 4.62 |
| 22:00 | 1398 | Burnley U23 vs Fulham U23 | 3.18 | 3.95 | 1.88 |
| 22:00 | 2708 | Colchester U23 vs Millwall U23 | 2.75 | 3.71 | 2.14 |
| 22:00 | 3484 | Beerschot Wilrijk U21 vs Lierse SK | 2.26 | 3.57 | 2.65 |
| 22:00 | 4164 | Excelsior Virton U21 vs Mouscron U21 | 4.33 | 4.24 | 1.58 |
| 22:00 | 4397 | Union Saint Gilloise U21 vs AS Eupen U21 | 5.41 | 4.73 | 1.42 |
| 22:00 | 5339 | Reading U23 vs Aston Villa U23 | 3.28 | 3.96 | 1.84 |
| 22:00 | 5955 | Lommel U21 vs Kmsk Deinze U21 | 2.70 | 3.57 | 2.23 |
| 22:30 | 1751 | RWD Molenbeek U21 vs Kortrijk U21 | 2.28 | 3.80 | 2.80 |
| 22:30 | 2265 | CA Boston River vs CA Progreso | 2.04 | 3.37 | 3.18 |
| 22:45 | 1557 | Dagenham and Redbridge vs Salford City | 3.34 | 3.54 | 2.03 |
| 22:45 | 3485 | NewellS Old Boys vs Union Santa Fe | 2.89 | 3.03 | 2.36 |
| 22:45 | 5553 | Concarneau vs Sedan | 1.75 | 3.24 | 4.91 |
| 23:00 | 1753 | Tenerife vs Girona | 2.13 | 3.14 | 3.43 |
| 23:00 | 2677 | AC Marinhense vs GD Peniche | 1.66 | 3.43 | 4.83 |
| 23:00 | 5257 | Cesena vs Pescara Calcio | 2.08 | 3.27 | 3.52 |
| 23:10 | 4714 | Ferro CO vs Santamarina | 1.50 | 3.66 | 6.17 |
| 23:15 | 1102 | Viseu vs CD Feirense | 2.73 | 3.08 | 2.54 |

### JUMANNE - 09 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1071 | Club Cortulua vs Real Cartagena | 1.64 | 3.57 | 4.73 |
| 00:00 | 5992 | Antofagasta vs La Serena | 1.97 | 3.43 | 3.33 |
| 00:15 | 4189 | Olimpia Asuncion vs Sportivo Luqueno | 1.68 | 3.81 | 4.15 |
| 00:45 | 2536 | Mvo Wanderers vs Cerro Largo FC | 2.28 | 3.23 | 2.84 |
| 01:00 | 3945 | Huracan vs Argentinos Juniors | 2.29 | 2.99 | 3.04 |
| 02:00 | 2125 | Chapecoense vs Flamengo | 8.08 | 4.71 | 1.31 |
| 02:00 | 2736 | Avai vs CSA AL | 2.01 | 3.04 | 3.67 |
| 02:30 | 2273 | Union Espanola vs CD Palestino | 3.43 | 3.53 | 1.90 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Novemba 8, 2021

Nipashe




Solskjaer: Man Utd itarudi kwenye ubora

UKURASA 21

## Makipa 10 waliookoa penalti nyingi EPL



**LONDON,** England

LIGI Kuu Egland imekuwa ikipambwa na magolikipa wengi bora kwa miaka mingi...

HABARI UK. 12

## Ancelotti amtabiria makubwa Xavi Barca

**MADRID,** Hispania



KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anatarajia Barcelona kurudi kwenye kiwango chake baada ya...

HABARI UK. 23



Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco. **PICHA: MTANDAO**

# KOCHA FRANCO KUVUNA SH. MILIONI 768/- SIMBA

### ●●● Kutambulishwa kesho, aeleza alivyomchapa Zidane na Real Madrid yake akiinoa Getafe, bonasi...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu mpya wa Simba, Pablo Franco, akitarajiwa kutua nchini leo kabla ya kutambulishwa kesho na kuanza kazi mara moja, ataigharimu timu hiyo Sh. milioni 768 kama mshahara wake tu, kwa kipindi cha mkataba wa miaka miwili atakaosaini, imefahamika.

**Franco ambaye ni mzaliwa wa jijini Madrid, Hispania, mbali na mshahara huo pia atavuta jumla ya Sh. milioni 138 kwa mwaka kama bonasi endapo atatimiza malengo yake aliyowekewa na waajiri wake hao.**

Kwa mujibu wa taarifa za ndani zilizolifikia Nipashe jana, Franco atakuwa akilipwa Dola za Marekani 14,000 kwa mwezi sawa na Sh. milioni 32 za Tanzania huku pia akigharamiwa tiketi ya ndege ya kurejea kwao na kurudi nchini.

"Bonasi atakazopata ni Sh. milioni 23 endapo atatwaa ubingwa wa Ligi Kuu, na kiasi kama hicho endapo ataiwezesha timu kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini atalipwa Sh. milioni 46 akituwezesha kufika nusu fainali ya michuano hiyo na tukifika fainali atalipwa pia bonasi ya Sh. milioni 46," kilieleza.

Franco mwenye umri wa miaka 41, ana leseni ya UEFA-Pro na anatua Simba akitokea Al-Qadsia ya Kuwait, lakini amewahi kuwa kocha msaidizi wa Real Madrid mwaka 2018 pia akiifundisha Getafe ya Ligi Kuu Hispania mwaka 2015.

"Miaka saba iliyopita, nilipata ushindi wangu wa kwanza kama kocha mkuu katika Uwanja wa Alfredo Di Stefano, kwa kuifunga Real Madrid Castilla ikinolewa na #Zidane [Zinedine]. Kumbukumbu nzuri," Franco ameandika katika mtandao wake wa twitter akiambatanisha picha wakiwa na Zinedine Zidane.

Katika hatua nyingine kikosi cha Simba kinaingia kambini leo na kuanza programu rasmi ya mazoezi na wachezaji waliopo baada ya baadhi kujiunga na timu zao za taifa kuelekea michuano ya kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Simba inatarajiwa kuendelea na mazoezi hayo baada ya kutoka katika mapumziko ya siku tatu huku wakitarajiwa kuanza kupata mbinu mpya kutoka kwa Franco ambaye anakuja kuchukuwa mikoba ya Mfaransa Didier Gomes.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema kocha huyo mpya ataungana na timu hiyo ndani ya wiki hii kuanzia atakapowasili na kuanza kazi rasmi ya kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Wakati huo huo, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Thierry Hitimana, alisema leo wataendelea na mazoezi baada ya mapumziko mafupi waliyokuwa wamepewa wachezaji ili kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu raundi ya sita itakayoendelea baadaye mwezi huu.

Alisema mazoezi yatakuwa ni ya kawaida na ndiyo yatampa taswira ya programu yake ambapo kesho wataanza mazoezi ya gym na jioni kwenda uwanjani huku akiwajumuisha na wachezaji kutoka kikosi cha U-20.

"Kesho (leo), tutaendelea na mazoezi, tutaanzia gym asubuhi na jioni tutamaliza uwanjani, kuwaweka fiti wachezaji ambao hawako katika majukumu na timu za taifa," alisema Hitimana.

Alisema kwa sasa hajapewa taarifa ya mabadiliko yoyote kuhusu ujio wa Kocha Mkuu (Pablo Franco), hivyo ataendelea na programu yake hadi hapo atakapowasili mrithi huyo wa Gomes.

Hitimana alisema mikakati yake kipindi hiki, nikuona Simba inapambana kurejea kwenye kiwango bora zaidi msimu huu wakati ikiwa imeshacheza mechi tano na kushinda tatu, kupata sare mbili ikikamata nafasi ya pili kwenye msimamo.

"Tumeona mechi tano tumecheza kwa presha kubwa sana, tunahitaji kutumia hizi siku za Kalenda ya Fifa kupunguza presha hiyo kwa wachezaji waliobaki, pia kujifua zaidi kwa ajili ya mechi yetu dhidi ya Ruvu Shooting ambayo tutacheza Novemba 19, mwaka huu," alisema Hitimana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >